# Nipashe

Ijumaa Januari 17, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580130

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710



## Waziri akuta kondomu zikiwa zimeanikwa juani hospitalini

UKURASA 3



Ukurasa 16
Meneja wa Bandari 24 za Viktoria na simulizi ya kukokotoa bil. 2/-

Ukurasa 15
Huu hapa ujasiriamali na ubunifu wake ulivyo

BUFE

Ijumaa Januari 17, 2020
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ukurasa 14
Marekani, China walipotia saini kuweka sawa mauzo biashara zao

Meneja wa Bandari 24 za Viktoria na simulizi ya kukokotoa bilioni 2/-

Na Elizabeth Zaya, MWANZA

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) katika bandari zake za Ziwa Viktoria, imejipanga kuzitumia kuleta mapinduzi ya kiuchumi.

Miongoni mwa mipango iliyojiwekea katika kufikia malengo hayo, ni kwenda sambamba na uboreshaji unaofanyika katika bandari zote zilizopo Ziwa Victoria.

Meneja wa Bandari hizo, Morris Mchindiuza, anasema tayari wameshatumia Sh. bilioni 16.5 katika miradi yake ya kimkakati kuboresha miundombinu ya Bandari za Ziwa Viktoria, ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Anasema kiasi hicho cha fedha, kimetumika katika kipindi cha miaka miwili lengo, dira kuu ni kuziongezea uwezo bandari hizo ambazo ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi, ndani ya safari kuelekea uchumi wa kati kitaifa.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI
Habari katika picha

Ukurasa 17

UKURASA 13

# Bashiru: Kuongoza maoni si tiketi kuteuliwa kugombea

**AWASHUSHIA** rungu wanaojipitisha na kutoa mlungula, asema dawa yao imeiva...*Endelea ukurasa wa 2*



## TAHADHARI MVUA KUBWA, UPEPO SIKU 4

UKURASA 2

Vijana wakitumia mkokoteni kuvusha watu kwa ujira wa Sh. 500, kwa mtu mmoja, baada ya mafuriko kuizingira Barabara ya Kawawa, eneo la Kinondoni Mkwajuni, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jijini Dar es Salaam jana. Picha ndogo: Mkazi wa Tandale kwa Mtogole, akiondoa maji yaliyojaa ndani ya nyumba anayoishi. **PICHA: SELEMAN MPOCHI**



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store

## Baba matatani kwa tuhuma za mauaji ya mtoto wake

UKURASA 3

**MICHEZO** MAXIME ASHUKURU KUFUTA LAWAMA ZA KUIBEBA YANGA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akisaini kitabu cha maombolezo, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mfalme wa Oman, Hayat Qaboos bin Said, katika Ofisi ya Ubalozi wa Oman, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Balozi wa Oman nchini, Ali Bin Almahroqi. **PICHA: OMR**

# Bashiru: Kuongoza maoni si sifa kuteuliwa kugombea

**Na Dege Masoli,**
MUHEZA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amemaliza pumzi za wanachama waliojipanga kutumia fedha ili kushinda katika kura za maoni za ubunge na udiwani katika uchaguzi mkuu utakaofanyika baadaye mwaka huu.

Katika kuweka sawa jambo hilo, Dk. Bashiru amesema mchakato wa kuwapata wanachama watakaopeperusha bendera ya chama hicho, hautaangalia aliyeongoza kura za maoni.

Akizungumza katika mikutano yake na viongozi na wanachama CCM juzi wilayani Pangani na Muheza, alisema mchakato wa kumpata mgombea wa kukiwakilisha chama kwenye uchaguzi huo licha ya kuanzia ngazi za kata na wilaya, kuna ngazi za uamuzi wa mwisho.

Bashiru ambaye aliwanyooshea vidole watia nia wa ubunge na udiwani ambao wameshaanza kujipitisha kwenye maeneo mbalimbali, alisema hatua hiyo haitawasaidia kwa kuwa majina yao yatachujwa mkoani na taifa ambako zitaangaliwa sifa zingine zaidi ya matokeo ya kura za maoni.

"Kura za maoni ni sehemu tu ya utaratibu, lakini si sifa mama kwa mwombaji wa nafasi ya ubunge ama udiwani. Unaweza kuongoza kwa kuhonga wajumbe, mtu huyo hatufai kwa kuwa wajumbe hao si wapigakura.

Kinachoangaliwa pamoja na mambo mengine ni kukubalika kwake kwa wananchi ambao ndio watakaomchagua," alisema.

Pia alisema kama mwanachama aliyeongoza ni chaguo la wajumbe kwa maslahi yao binafsi, kikao cha mkoa au taifa kitarejesha jina la mtu mwingine atakayeonekana anakubalika kwa wananchi hata kama katika mchakato wa kura za maoni za chama alipata sifuri.

Alisema lengo ni kukipunguzia mzigo chama wa kuwa na wagombea wasiokubalika kwa wapigakura ambao huwa chaguo la wajumbe waliohongwa na kwamba mizengwe hiyo imekigharimu chama ikiwamo kutumia nguvu kubwa kuwanadi baada ya wagombea wanaokubalika kwenda upande wa pili ambako wengi wao huibuka washindi.

Katibu mkuu huyo alihimiza uadilifu kwa viongozi wa chama katika mchakato mzima wa kuteua wagombea na kuwataka kutoa kipaumbele kwa maslahi ya taifa badala ya kuangalia maslahi binafsi.

# Tahadhari mvua, upepo mkali siku 4

**Na Waandishi Wetu**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA), imetoa tahadhari kuwapo mvua kubwa kuanzia jana na upepo mkali kwa baadhi ya maeneo ya mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Zanzibar na Pwani hususani kisiwani Mafia.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, kuanzia jana hadi Jumapili, kunatarajiwa kuwapo upepo mkali na mawimbi makubwa kwa baadhi ya maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi, hivyo kusababisha shida kwenye uvuvi na usafiri wa baharini.

"Kiwango cha mvua na upepo in cha wastani, hivyo wananchi wachukue tahadhari katika shughuli zao," TMA ilieleza katika taarifa yake hiyo.

Ilisema athari huenda zikajitokeza kutokana na kusimama kwa shughuli za binadamu, kuharibika kwa miundombinu na makazi kuzingirwa na maji, hivyo kuna haja kuchukua tahadhari.

Mamlaka hiyo ilisema mvua inayonyesha sasa ni mwendelezo wa utabiri wa mvua za vuli iliotoa kipindi cha nyuma na katika baadhi ya maeneo itaendelea hadi mwezi ujao.

**DAR 'YAZAMA' TENA**

Wakati TMA ikitoa hadhari hiyo, mvua inayoendelea kunyesha nchini, imesababisha baadhi ya shughuli kusimama katika Jiji la Dar es Salaam.

Mvua iliyonyesha jana alfajiri jijini humo, ilisababisha kusitishwa kwa usafiri katika maeneo ya jiji hilo la kibiashara kutokana na maji kutuama barabarani.

Maeneo yaliyoathirika ni pamoja na Kariakoo, Kigogo na Kinondoni, ambako kulishuhudiwa magari yakiwa yamesimama kwenye foleni kwa muda mrefu.

Pia baadhi ya watu walilazimika kuyahama kwa muda makazi yao kutokana na kuzingira na maji, huku baadhi wakionekana kukaa juu ya paa kuokoa maisha yao.

Katika maeneo ya Kinondoni Mkwajuni, Nipashe ilishuhudia baadhi ya vijana wakitumia fursa ya kunyesha kwa mvua hiyo kujipatia kipato kwa kuvusha watu kutoka upande mmoja wa barabara kwenda mwingine kwa kutumia matoroli.

***Imeandikwa na Faustin Feliciane na Enock Charles**

# TCRA yawatoa hofu wananchi laini za simu zitakapozimwa

**Na Waandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imewatoa hofu watu ambao hawatakuwa wamesajili laini zao kwa alama za vidole ifikapo Januari 20, kuwa jambo hilo ni endelevu.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa kwenye vyombo vya habari jana na kutiwa saini na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, TCRA iliwatoa hofu wananchi watakaofungiwa laini zao. "Kwa watakaositishiwa huduma za laini zao za simu Januari 20, wanaweza pia kuendelea na utaratibu wa usajili kwa lengo ama kurudisha laini zao zitakazokuwa zimefungwa au kupata laini mpya. Zoezi hili ni endelevu.

"Kwa watumiaji/waombaji wa laini za simu, wataendelea kusajiliwa muda wote na usajili huo kwa kutumia kitambulisho cha taifa na kuhakikiwa kwa alama za vidole," ilifafanua.

Mamlaka hiyo pia ilisema kuwa wanadiplomasia au taasisi zao ambao hajakamilisha usajili, wanatakiwa kufuata utaratibu uliowekwa.

**WAOMBA MUDA ZAIDI**

Wakati TCRA ikiyasema hayo, baadhi ya wakazi wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, wameiomba serikali kuongeza muda wa usajili kutokana na wengi kukosa namba za kitambulisho cha taifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida).

Wakizungumza katika Uwanja wa Kaitaba, ambako Nida imeweka kambi kuhudumia wananchi ambao bado hawajapata vitambulisho au namba, baadhi ya wakazi hao walisema jana kuwa wamekuwa wakizungushwa mara kwa mara bila mafanikio.

Mmoja wa wananchi hao, Catherine Paulo (59), alidai alijaza fomu na kuikabidhi Nida Oktoba 17 mwaka jana, lakini tangu wakati huo hadi sasa hajapata kitambulisho hicho wala namba. "Baada ya kukabidhi fomu niliambiwa nisubiri zipite wiki tatu ndipo nirudi, niliporudi nilitakiwa kuondoka na kuambiwa nirudi tena baada ya wiki mbili, lakini cha kushangaza hadi sasa sijapata chochote, nazungushwa tu nashindwa kufanya shughuli zangu za kuniingizia kipato, hata leo sijui wapi nitapata chakula," alilalamika.

Ofisa Msajili kutoka Nida Wilaya ya Bukoba, Hassan Godigodi, alisema wanajitahidi kila mwenye haki ya kupata namba apate kwa wakati.

Kutokana na Mkoa wa Kagera kupakana na nchi nyingi, ilielezwa kuwa baadhi ya wananchi hawajapata namba kutokana na uraia wao kuwa na utata. Ofisa Uhamiaji wa Mkoa huo, Pendo Buteng'e, alikiri kupokea watu kwa ajili ya kuhakikiwa taarifa zao za uraia, akisisitiza kuwa ni lazima wajiridhishe kama wanaoomba vitambulisho ni raia wa Tanzania au la.

Alisema hadi sasa, kuna baadhi ya watu wamechukuliwa hatua ikiwamo kufikishwa katika vyombo vya sheria na baadhi yao kurejeshwa katika nchi zao, baada ya kubainika kujiandikisha ili wapate kitambulisho cha taifa wakati si raia.

Hata hivyo, ofisa huyo hakuwa tayari kuweka wazi idadi ya watu ambao wamechukuliwa hatua hizo.

Alisema wananchi wanapaswa kuelewa uandikishaji kwa ajili ya kupata kitambulisho ni endelevu.

**●Imeandikwa na Salome Kitomari (DAR) na Lilian Lugakingira (BUKOBA)**

## HABARI KITAIFA

# Waziri akuta kondomu zikiwa zimeanikwa juani hospitalini

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, ameamuru Jeshi la Polisi kuwakamata watumishi wawili wa Hospitali ya Wilaya ya Rungwe kwa tuhuma za kufanya 'madudu' hospitalini, ukiwamo wizi wa dawa na utunzaji mbovu wa baadhi ya dawa na vifaa tiba.

Watumishi hao ni Ofisa Ununuzi wa Hospitali hiyo, Vumilia Mwaijande, na Mfamasia wa Hospitali hiyo, Eliah Kandonga, ambao alibaini wanatoa dawa za hospitali hiyo bila kuweka kumbukumbu za aina yoyote na hivyo kuhisiwa kuiba dawa hizo.

Katika ziara yake ya kushtukiza hospitalini hapo jana, Naibu Waziri huyo alikutana na kituko kingine cha Mfamasia wa Hospitali hiyo, Kandonga, kuanika kondomu juani kwa madai kuwa anataka kuzirejesha katika hali yake ya kawaida baada ya kubaini zinaharibika.

Dk. Ndugulile alisema ni kosa kubwa kuhifadhi kondomu kwa mtindo huo kwa kuwa zinaharibika na hata kuwa chanzo cha ongezeko la maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VVU) mkoani humo.

Naibu Waziri huyo alisema aliamua kufanya ziara ya kushtukiza hospitalini hapo baada ya kupata taarifa za siri kuwa kuna mambo yanayofanyika kinyume cha taratibu. Akiwa katika chumba cha kuhifadhia dawa, Naibu Waziri huyo alibaini baadhi ya nyaraka za dawa zinaonyesha kuna dawa 50 ndani ya chumba hicho, lakini alipohesabu, alibaini ziko 30, huku kukiwa hakuna nyaraka ambazo zinaonyesha kuwa baadhi ya dawa zilitolewa na haielezwi zilikopelekwa.

Alipomhoji Ofisa Ununuzi wa Hospitali hiyo, Mwaijande, aliyekutwa anasimamia chumba hicho badala ya mfamasia, alieleza kuwa dawa hizo zilikuwa zimetolewa na kupelekwa kwa wagonjwa bila kuandikwa popote.

Maelezo hayo yalimkera Naibu Waziri na akaamuru wakamatwe na kuwekwa selo kwa ajili ya mahojiano juu ya utendaji wao wa kazi na kujua walikozipeleka dawa hizo.

"Nakuagiza Mganga Mkuu wa Mkoa, uunde timu ije hapa ichunguze mtiririko wa uingizwaji na utolewaji wa dawa katika hospitali hii kwa kipindi cha mwaka mzima, maana hapa inaonekana kuna wizi wa dawa za serikali," aliagiza.

Pia alimtaka Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salumu Manyata, kumwondoa mara moja Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Rungwe, Dk. Manase Ngogo, kwa sababu ya usimamizi mbovu wa hospitali.

Alisema kiongozi huyo ameshindwa kusimamia nidhamu ya watumishi kwa maelezo kuwa wakati anaingia katika hospitali hiyo, alikuta baadhi ya watumishi wakizurura barabarani muda ambao walitakiwa wawe wanawahudumia wananchi.

"Huyu Mganga Mfawidhi anaonekana hana uwezo wa kutimiza majukumu aliyopewa, sasa ni vyema abadilishwe ili wananchi wapate huduma bora wanazostahili," aliagiza.

Katibu Tawala Wilaya ya Rungwe, Mnkondo Bendera, alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo itashauriana ili kuchukua hatua stahiki kwa yeyote aliyehusika na uzembe katika hospitali hiyo.

Alisema baadhi ya vitu vinavyotendeka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, ukiwamo wizi wa dawa, ndivyo vinawafanya wananchi wakose imani na serikali yao. Awali, Naibu Waziri alikutana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila ambaye alimweleza kuwa katika mkoa huo kuna tatizo la wizi wa dawa unaofanywa na baadhi ya watumishi ambao si waaminifu.

Chalamila alisema malalamiko mengi ya wizi wa dawa hizo huwa yanatoka katika Wilaya ya Rungwe ambako ndiko Naibu Waziri alibaini 'madudu' hayo.

# Baba matatani tuhuma za mauaji ya mwanawe

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamshikilia Juma Daniel (30), mkazi wa Kijiji cha Kazingata Kata ya Keza wilayani Ngara mkoani humo, kwa tuhuma za mauaji ya mwawe.

Imeelezwa kuwa mtoto huyo Bahati Juma (2), alikutwa na mauti baada ya baba yake kumpa kichapo na kumjeruhi sehemu mbalimbali, ikiwa ni adhabu ya kujisaidia kitandani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alisema tukio hilo lilitokea Januari 14, mwaka huu majira ya jioni, na kwamba Bahati alifariki akiwa njiani kupelekwa hospitali.

Kamanda Malimi alisema wanamshikilia mtuhumiwa huyo kwa kosa la mauaji ya kukatili.

Alisema Daniel alikuwa amelala na Bahati kitanda kimoja, na baada ya kujisaidia kitandani ndipo alianza kumwadhibu kwa kumchoma moto usoni na makalioni kisha kumjeruhi na kitu chenye incha kali sehemu za haja kubwa.

Aidha, Malimi alisema baada ya kufanya kitendo hicho Desemba 27, mwaka jana hakumpeleka hospitali bali alianza kumtibu majeraha kwa dawa za kienyeji nyumbani kwake.

Hata hivyo, alisema baada ya mtuhumiwa kuona hali ya mwanawe inakuwa mbaya ndipo alipoamua kutoroka kusikojulikana hadi majirani walipotoa taarifa kwa viongozi wa kijiji.

Aliongeza kuwa baada ya majirani kubaini mtoto huyo amefanyiwa ukatili huo, Januari 14, mwaka huu walimpeleka hospitali, lakini alipoteza maisha wakiwa njiani.




# Upasuaji bila kufumua fuvu mwezi ujao MOI

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa (MOI), inatarajia kuanza kutoa huduma za upasuaji wa matatizo ya mishipa ya damu kichwani bila kufungua fuvu la kichwa kuanzia mwezi ujao.

Imeelezwa kuwa katika kutekeleza mpango huo, serikali ilitoa Sh. bilioni 7.9 kwa ajili ya kujenga maabara ya kisasa ya upasuaji wa ubongo itakayokuwa na mashine yenye uwezo wa kutibu damu iliyoganda kwenye mishipa ya damu miguuni.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, aliyaeleza hayo wakati akizungumzia mafanikio ya miaka minne ya taasisi hiyo katika ziara ya maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, walipoitembelea kuangalia mafanikio hayo jana jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwapo kwa maabara hiyo kutaifanya Tanzania kuwa moja ya nchi chache barani Afrika zinazotoa huduma hiyo.

"Mwezi Mei mwaka jana, serikali ilitoa Sh. bilioni 7.9 ili kujenga maabara hii ya kisasa, itakayosaidia upasuaji wa mishipa ya damu katika ubongo.

"Kwa sasa, tunafanya upasuaji kwa kufungua ubongo, lakini kuanzia Februari 15 mwaka huu, tutaanza kufungua mashine hizi za kisasa na kutoa huduma hii kwa njia ya kisasa," alisema.

Dk. Boniface aliongeza kuwa watafanya upasuaji huo kwa kupitisha vifaa kwenye mishipa ya damu na kuingia kwenye ubongo moja kwa moja na kutibu tatizo kwa muda mfupi na kwa haraka.

Mkuu wa Kitengo cha Radiolojia wa MOI, Dk. Mechris Mango, alisema mitambo ya kisasa ya kutoa huduma katika maabara hiyo imeshawasili nchini na wanasubiri kukamilika kwa ujenzi wa chumba maalum cha kuifunga ili kuanza kutoa huduma hiyo.

Dk. Mango alisema kuwapo kwa maabara hiyo kutasaidia kupunguza rufani za kwenda nje ya nchi kupata matibabu hayo.

Alisema watakaopatiwa matibabu ni wagonjwa wenye uvimbe wa mishipa ya damu kichwani ili kusaidia kutambua ni mshipa upi unapaswa kufungwa ili kuondoa uvimbe.

Awali, Dk. Boniface akizungumzia mafanikio ya miaka minne ya uongozi wa Rais John Magufuli katika taasisi hiyo, alisema kuwapo kwa miundombinu ya kisasa kumesaidia kuongeza wagonjwa wa upasuaji kutoka 500 kwa mwezi hadi 900 kwa mwezi.

Alibainisha kuwa jumla ya wagonjwa 43,200 wamefanyiwa upasuaji mbalimbali katika taasisi hiyo, ukiwamo upasuaji wa nyonga 900, magoti 870, mfupa wa kiuno 618, ubongo 880 na watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi 2,070.

Dk. Boniface alisema gharama za matibabu hayo ndani ya nchi zilikuwa Sh. bilioni 16.5 na kama wangetibiwa nje ya nchi wangetumia Sh. bilioni 54.9, hivyo wamesaidia kuokoa Sh. bilioni 38.4.

Pia, alisema wamefanikiwa kuanzisha huduma za upasuaji wa magoti na mabega kwa njia ya matundu na wagonjwa 800.

Alitaja mafanikio mengine kuwa ni kuondoa vivimbe vya mishipa ya damu kwenye ubongo kwa wagonjwa watano, kunyoosha vibiongo kwa watoto 12 na upasuaji wa uti wa mgongo kwa kupitia tundu dogo kwa wagonjwa 120.

Alisema katika kipindi hicho wameanzisha wodi maalum ya kulazwa na kufanyiwa upasuaji siku hiyo hiyo na wagonjwa 335 wamehudumiwa na huduma ya dawa za usingizi pasipo kulala na wagonjwa 250 walinufaika na hivyo kuwezesha huduma muhimu za matibabu kutolewa nchini kwa asilimia 95.



Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood (wa pili kulia), akipata maelezo ya mradi wa ujenzi wa soko kuu la kisasa la mkoa huo, kutoka kwa Mhandisi wa Manispaa ya Morogoro, Juma Uwiso (wa pili kushoto), alipotembelea mradi huo, jana, unaogharimu Sh. bilioni 17. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Mbaroni tuhuma mauaji ya wanandoa

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WATU saba wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Kagera, wakituhumiwa kuwaua wanandoa wawili kwa kuwakata sehemu mbalimbali za miili yao, chanzo kikidaiwa kuwa ni mgogoro wa ardhi.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa tukio hilo lilitokea Januari 14 mwaka huu saa saba usiku katika Kijiji cha Mabale, Kata ya Nyakahura wilayani Biharamulo.

Alisema kuwa wakati wanandoa hao wakiwa wamelala, mlango wa nyumba yao ulivunjwa na kuvamiwa na kundi la watu ambao hawakufahamika na kuanza kuwakata kwa kitu chenye ncha kali sehemu mbalimbali za miili yao na kusababisha kupoteza maisha papo hapo.

Aliwataja waliouawa katika tukio hilo kuwa ni Elizeus Rubanie (35) na mke wake, Juliana Joseph (28).

"Kabla ya tukio hilo, kulikuwa na mgogoro wa ardhi kati ya marehemu na baadhi ya wanaukoo kwa muda mrefu, uliotokana na kuachiwa eneo alilokuwa akiishi na babu yake, aliyehama kwa shinikizo la wanajamii waliomtuhumu kuwa ni mwizi," alidai.

Kamanda Malimi alidai kuwa baada ya babu huyo kuhama na kumwachia eneo hilo mjukuu wake, baadhi ya wanajamii waliungana na baadhi ya ndugu kwenye ukoo huo, hasa shangazi wawili wa marehemu, na kuanza kumsakama marehemu na familia yake na kumtolea vitisho.

"Walimtaka ahame kwenye shamba hilo wakidai hana haki ya kumiliki ardhi hiyo, mgogoro ambao umekuwa ukisuruhishwa kwa muda mrefu na viongozi wa serikali ya kijiji," alidai.

Aliwataja wanaoshikiliwa kuwa ni Sophia Joseph (45), Joseph Magambo (47), Alphonce Karoli (37), Martine Makabe (36), Alex Leopord (44), Salvatory Mwiliza (38) na Aloyce Leopord (45).

Kamanda Malimi alidai upelelezi bado unaendelea ili kubaini watu wote waliohusika na tukio hilo, na kuwa watuhumiwa watafikishwa mahakamani wakati wowote baada ya upelelezi kukamilika.

# OPEC wakoshwa miradi ya Tasaf

**Na Elizabeth Zaya,** ARUSHA

OFISA Uendeshaji Mkuu wa Mfuko wa Misaada kutoka nchi zinazozalisha na kusambaza mafuta duniani (OPEC), Shoragim Shams, ameupongeza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), kwa kusimamia vyema fedha za miradi zinazotolewa na mfuko huo.

Shams alitoa kauli hiyo jana mjini Arusha katika ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya elimu katika Shule ya Sekondari Oldonyowas katika Kijiji Cha Oldonyowas mkoani Arusha.

Alisema utoaji fedha za miradi ni jambo moja, lakini utekelezaji ni jambo jingine ambalo Tasaf wamefanikisha kuhakikisha zinatumika kama ilivyokusudiwa.

"Sisi tumetoa fedha kwa lengo la kusaidia jamii, lakini zisingeweza kusaidia chochote endapo kusingekuwapo usimamizi thabiti na wananchi wenyewe kujitolea nguvu zao.

"Nimetembelea na kushuhudia kilichofanyika ni kizuri na OPEC tunaipongeza Tasaf na kuahidi kuendeleza kushirikiana nanyi katika awamu nyingine inayofuata," aliahidi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tasaf Taifa, Ladislaus Mwamanga, alisema mwakilishi huyo wa OPEC amekuja kuangalia utekelezaji wa miradi hiyo awamu inayomalizika kwa lengo la maaandalizi ya awamu nyingine inayotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Alisema katika awamu inayomalizika, mambo mengi yamefanyika kwa ufadhili wa wadau hao katika maeneo ya uboreshaji miundombinu ya elimu, afya, maji na barabara.

"Katika Shule hii ya Sekondari Oldonyowas zaidi ya Sh. milioni 470 zimetumika katika ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, mabweni na matundu ya vyoo," alisema.

Mwamanga aliwapongeza wananchi kwa kujitoa katika nguvu kazi na kusisitiza utekelezaji wa miradi unahitaji ushirikiano na wananchi ili kuzalisha ajira za muda zitakazojitokeza.

Diwani wa Olturoto, Baraka Simon, alisema kukamilika kwa ujenzi wa mabweni hayo, kutasaidia wasichana 96 na kuwaondolea vikwazo vya kutembea umbali mrefu wa kilometa 12 kufika shuleni hapo.

"Ni furaha kwetu lakini tunaomba awamu ijayo mtufikirie kujenga hata madarasa ya kidato cha tano na sita ili wanafunzi wetu wakimaliza kidato cha nne wasihangaike kwenda mbali," aliomba.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Oldonyowas, Geoffrey Ayo, alisema wametekeleza miradi sita ya kupunguza umaskini kupitia miradi hiyo ya OPEC na serikali.

Alisema miradi hiyo pia imewasaidia wanufaika wa Tasaf kupata ajira za muda na kuwapunguzia umaskini.

Alisema hadi sasa miradi minne imekamilika na mabweni mawili yako katika hatua za mwisho kukamilika.

"Tunashukuru Mungu kwa sasa wanakijiji wamejikwamua kiuchumi kupitia miradi hii, huku wengine wakiibua na kuendeleza mradi wa ufugaji kuku na ng'ombe ambao umeleta mafanikio makubwa," alisifu.

# Wakulima walipwa bil. 68/- za korosho

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

WAKULIMA wa zao la korosho wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima Masasi-Mtwara (MAMCU) tawi la Masasi, wameshalipwa zaidi ya Sh. bilioni 68.2 za korosho kupitia minada tisa iliyofanyika hadi sasa.

Hayo yalibainishwa na Meneja wa MAMCU tawi la Masasi, Joseph Mmole, alipokuwa akizungumza na gazeti hili, kuhusu malipo ya zao la korosho kwa msimu wa 2019/2020.

Mmole alisema zaidi ya kilo milioni 47.3 za korosho za wakulima wa vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) katika Wilaya ya Masasi na Nanyumbu zimeuzwa kwenye jumla ya minada tisa.

Alisema katika minada hiyo tisa iliyofanyika kwa vipindi tofauti, wakulima hao wamelipwa zaidi ya Sh. bilioni 68.2 hadi sasa.

Mmole alisema malipo hayo kwa sehemu kubwa wamelipwa wakulima wa vyama vya msingi vilivyopo katika eneo la Halmashauri ya Mji Masasi pamoja na wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Alisema kwa mnada wa tisa na wa kumi, wakulima wameanza kulipwa fedha zao ambapo awali malipo hayo yalikuwa yamechelewa kidogo kwa sababu mbambali.

"Tunashukuru sana kwani katika misimu ya korosho ambayo tumefanya vizuri katika malipo ya korosho kwa wakulima ni wa 2019/ 2020 kwa sababu wakulima wengi wamelipwa fedha zao vizuri bila misuguano ya aina yeyote," alisema Mmole.

Alisema katika kuelekea kufunga msimu wa korosho 2019/2020, vyama 87 vya wilaya za Nanyumbu na Masasi vyama 41 kati ya hivyo vimeshafunga msimu kwa sababu kwenye maeneo yao korosho zimekwisha.

Mmole aliongeza kuwa ni vyama 46 pekee kati ya hivyo ndivyo hadi sasa vinaendelea kukusanya korosho za wakulima na kuzipeleka katika maghala makuu kwa ajili ya kusubiri minada kuziuza.

Alisema hadi sasa korosho za wakulima ambazo hazijaingizwa katika maghala makuu kutoka kwa wakulima ni kilo zaidi ya milioni 1.4, na kwamba muda wowote korosho hizo zitaingizwa katika maghala makuu kuuzwa.

Mmole alisema kwa msimu huu wa 2019/2020 hakukuwa na changamoto zozote kubwa ambazo zilijitokeza na hiyo ni kutokana na viongozi wengi wa AMCOS kuzoea mfumo wa sasa ukilinganisha na msimu uliopita wa 2018/2019.

Naye Bakari Said, mkulima kutoka Wilaya ya Nanyumbu, aliipongeza serikali kwa usimamizi mzuri wa zao la korosho, na kwamba wakulima wanaendelea kulipwa fedha zao bila vikwazo.

# Walimu wakwamisha shule aliyochangia JPM

**Na Shaban Njia,** KAHAMA



SHULE ya Msingi Mayila iliyopo Kata ya Nyihogo Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, ambayo Rais John Magufuli (pichani) aliichangia Sh. milioni tano kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa, inakabiliwa na upungufu wa walimu.

Shule hiyo ilijengwa kwa nguvu za wananchi, Halmashauri na Ofisi ya Mbunge Jumanne Kishimba na kusajiliwa mwaka huu, na kuanza kufundisha wanafunzi ambao walikuwa wakitembea kilometa nne kwenda shule ya jirani ya Nyihogo.

Shedrack Nkwambi, Diwani wa Nyihogo, aliyabainisha hayo katika kikao cha kawaida cha baraza la madiwani, na kufafanua kuwa kwa sasa shule hiyo ina zaidi ya wanafunzi wa darasa la kwanza 360 na wanafunzi wa awali 140, huku ikiwa na walimu watatu tu, ambao hawawezi kuwafundisha wanafunzi wote, badala yake wanafunzi wanashinda wakicheza.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga Shule ya Msingi Mayila kwa ajili ya kupunguza vifo vya wanafunzi vilivyokuwa vikitokea hasa wakivuka barabara kuelekea Shule ya Nyihogo. Na tangu tumeifungua shule ina zaidi ya wanafunzi 360 kwa darasa la kwanza na 140 darasa la awali huku ikiwa na walimu watatu tu," alisema.

Naye Diwani wa Malungu, Shaban Suleiman, alisema shule za msingi na sekondari zimekuwa na migogoro ya mipaka ya maeneo, kuvamiwa na wananchi na kuendesha shughuli za kilimo au kujenga nyumba za makazi.

Hata hivyo, alisema ili kutatua migogoro hiyo, idara ya ardhi inatakiwa kuyapima upya maeneo yote ya shule kwa kuweka mipaka upya, na kuhakikisha zinatoa ramani za shule kwa madiwani ili wasimamie vyema.

Akijibu hoja hizo Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, alisema halmashauri ina uhaba wa zaidi ya walimu 600 wa shule za msingi na sekondari ikiwamo shule hiyo.

Alisema walimu 350 waliopo katika shule za msingi watahamishwa na kwenda kwenye shule zilizopo pembezoni mwa mji zenye uhaba wa walimu ili kukabiliana na uhaba wa walimu, na kwamba shule ya Majila itapatiwa walimu hivi karibuni.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF WATER
RURAL WATER SUPPLY AND SANITATION AGENCY

RUWASA

**Bid No.AE-102/2019/2020/CS/001**
**FOR**
**PROVISION OF TECHNICAL SUPPORT SERVICES TO RUWASA's ICT STAFFS IN DEVELOPMENT OF INFORMATION COMMUNICATION SYSTEM**

**EXPRESSION OF INTEREST (EOI)**

**Date: 17th January, 2020**

1. The Rural Water Supply and Sanitation Agency (RUWASA) has set aside funds for the recruitment of an Individual Consultant to provide technical support services to RUWASA's ICT Staffs in development of information communication system. It is intended that part of the proceeds of the fund will be used to cover eligible payment under the contract for the Consultancy Services on Provision of the technical support services to RUWASA's ICT Staffs in development of information communication system for the financial year 2019/2020.

2. The main objective of this assignment is to improve RUWASA's operational efficiency through technical support on web design and development of information Communication Systems by studying operations; leading design and, development of various ICT solutions to improve operational efficiency of RUWASA.

3. The Scope of service shall include but not limited to the following activities:
   i. Accessing the effectiveness of the existing ICT systems
   ii. Development of RUWASA ICT Policy and Strategy
   iii. Development of ICT solutions
   iv. Web Development and Management Digital Platforms
   v. System Administration and Security

4. The Rural Water Supply and Sanitation Agency (RUWASA) now invite eligible and qualified Individual Consultants to indicate their interest in providing the specified services. The interested Consultants must provide information indicating that they are qualified to perform the services by submitting their profiles, description of similar assignments, experience in similar conditions, availability of appropriate skills among staff, etc.

5. A consultant will be selected in accordance with the procedures set out in the Public Procurement Act No. 7 of 2011 and the Public Procurement Regulations – Government Notice No. 446 of 2013 together with their Amendments of 2016.

6. Selection to be short listed will be based on the required capabilities and experience for the improvements of RUWASA's operational efficiency through technical support on web design and development of information Communication Systems by studying operations; leading design and, development of various ICT solutions to improve operational efficiency of RUWASA.

7. Interested eligible consultants may obtain further information from the office of the Secretary, Tender Board, NBC Bank, Second Floor 2, PMU office, P.O.Box 412, Kuu Road, 40473, Dodoma from 9.30 AM on Monday to Friday 3:00 PM inclusive except on public holidays.

8. Expressions of Interest (EoI) in one original plus two copies must be enclosed in a sealed envelope properly addressed and delivered to the Secretary, Tender Board, NBC Bank, Second Floor 2, PMU office, P.O.Box 412, Kuu Road, 40473, Dodoma **at or before 11.30 am, 31st January, 2020.** The envelopes containing EoI must be clearly marked **"Expression of Interest for Provision of the technical support services to RUWASA's ICT Staffs in development of information communication system."**

9. Late Expressions of Interest shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**DIRECTOR GENERAL**
**RURAL WATER SUPPLY AND SANITATION AGENCY**

215587302

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Maofisa mikopo wa benki wadhibitiwe

**JUZI** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, aliwaonya baadhi ya maofisa mikopo wa benki mbalimbali nchini, ambao wamekuwa wakishirikiana na madalali kuuza mali za wananchi waliochukua mikopo.

Alikwenda mbali zaidi na kutoa mfano wa ofisa mikopo mmoja ambaye alijimilikisha nyumba tano za wananchi walikuwa na mikopo wakashindwa kuilipa.

Nyumba hizo alizipata kilaghai kwa kuwa wakopaji husika hawakupewa nafasi ya kujitetea au kuwa na mazungumzo na benki husika bali moja kwa moja ulifanyika mpango wa kuuza mali zao na mnunuzi akawa ofisa mikopo.

Waziri huyo alieleza kuwa maofisa mikopo wanapotoa mikopo kwa wateja husubiri mwaka mmoja kisha wanawafuata madalali, ambao hupewa kazi ya kwenda kupiga mnada mali iliyowekwa dhamana kwa madai ya mhusika kukiuka masharti ya mikopo.

Waziri anarudia kauli hiyo ambayo amekuwa akiisema mara kwa mara kwa kuwa lilikuwa tatizo kubwa ambalo linaendelea kwisha taratibu.

Mara ya kwanza aliwaonya madalali wanaokula njama na benki ili kuuza mali za wakopaji wanyonge kinyume cha sheria.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, mwaka 2016 alipokea malalamiki zaidi ya 80 ya kesi za watu walioonewa na madalali hao na kati ya kesi hizo zaidi ya asilimia 75 ni wanawake.

Alisema madalali hao wanachokifanya, wanakwenda siku ya Jumamosi Sinza wananadi nyumba kwa Sh. milioni 4 , na kwamba haiwezekani nyumba kuuzwa chini ya asilimia 25 ya thamani, huku akiwataka kufanyakazi hiyo kwa sura ya ubinadamu na si kuangalia fedha.

Tunafahamu katika kutafuta suluhisho la utakaokuwa na ulaghai huu, Waziri Lukuvi aliweka masharti kwamba bei wanayotaka kuuzia nyumba husika mthamini wa ardhi ni lazima ajue, hatua zilizofikiwa hadi kuuza nyumba ziandikwe na ziwe wazi ili kujua thamani halisi ya nyumba husika kulingana na bei ya soko.

Kinachotakiwa kufanyika ni mtathmini wa ardhi atafuatili kujua bei iliyouzwa kama ndiyo bei ya soko na kama haki imetendeka kabla ya kuhamisha umiliki wa nyumba.

Sambamba na hilo, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ilisema na kanuni za sheria ya fedha ambazo zitazibana taasisi za kifedha kuwa na utaratibu wa kuwasikiliza na kujadiliana na wateja ambao wameshindwa kulipa mikopo kutokana na kuporomoka kiuchumi. Alichokisema Waziri Lukuvi ndiyo uhalisia kutokana na vilio ni vingi na wengine wamepata maradhi ya shinikizo la damu kutokana na kupoteza mali zao katika mazingira ambayo wangeweza kuokoa mali zao na kulipa deni la benki.

Tunaona lipo tatizo la msingi ambalo benki zinapaswa kulishughulikia kabla ya kufanya mnada wa mali ya mteja wao, kama alivyoelekeza Waziri lazima kujiridhisha na mambo mengi ikiwamo mthamini wa ardhi kushirikishwa ili nyumba husika iuzwe kwa bei halisi na siyo kwa lengo jingine.

Tunaamini iwapo kutakuwa na mazunguzo na wateja kabla ya kufikia uamuzi wa kuuza mali husika, basi kutakuwa na maelewano na hatua za kisheria zitafuatwa na kila upande kuridhika kabla ya kuingia kwenye mvutano au uonevu wowote.

Lakini, benki zinapaswa kujisafisha juu ya lawama hizi kwa kuchukua hatua kwa wote ambao wameonekana kunufaika na mali za wakopaji ambazo zimepatikana kwa njia za dhuluma na ujanja unaoacha maumivu kwa wateja.

Tunazishauri benki kuweka utaratibu wa kuwafuatilia maofisa wake kimaadili kwa kuwa kuna mambo mengi yasiyofaa ambayo baadhi yao wamekuwa wakiyafanya likiwamo kuwaomba au kuwalazimisha wawape fedha wateja waliopata mikopo kwenye benki zao kwa madai kuwa wamewasaidia kuwezesha mchakato wa kukopeshwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Muda wa usajili laini simu uangaliwe upya

Na Salome Kitomari

**KWENYE** maeneo mengi nchini kwa sasa wananchi wanahangaika kupata namba za vitambulisho vya Taifa ili waweze kusajili laini zao kabla ya Januari 20, mwaka huu.

Tayari Mamlaka ya MawasilianoTanzania (TCRA), imetoa tangazo kusisitiza kuwa ifikapo Januari 20, laini zote ambazo hazijasajiliwa kwa alama za vidole zitafungwa na wahusika wataendelea kusajiliwa ndipo zitafunguka.

Usajili wa laini hauna kikwazo chochote kwa kuwa hakuna foleni na kampuni za simu zimejipanga ipasavyo, kwa kuwa kuna mashine ndogo zinazotumiwa na vijana wanaotembea hadi kwenye makazi ya watu kusajili laini za simu.

Kwa takribani miezi sita sasa changamoto kubwa imekuwa ni kupata namba ya utaifa kabla ya kitambulisho chenyewe, na wengi wanalilia kupata namba namba hizo kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali.

Wengi wameshajiandikisha na kupeleka viambatanisho muhimu, lakini wameambiwa wasubiri wiki tatu hadi nne ili kupata namba.

Yapo maeneo ambayo wananchi wanalazimika kusafiri umbali mrefu kupata huduma huyo, mathalani wananchi wanaoishi Ugweno mkoani Kilimanjaro, wanatakiwa kusafiri hadi Mwanga kujiandikisha kwa ajili ya kupata namba.

Kuna wakati Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) walikwenda Ugweno wakaandikisha watu na kuwataka kufuatilia namba, lakini hadi sasa hawajazipata, na wametakiwa kujiandikisha upya kwa kwenda wilayani.

Maana yake ni kuwa mwananchi anatakiwa kuwa na nauli na muda wa siku nzima kujiandikisha kwa ajili ya kupata namba itakayomwezesha kupata kitambulisho.

Takwimu za mara ya mwisho zilizotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) zilionyesha kuwa zaidi ya watu milioni 22, hawajajiandikisha, ambayo ni kubwa na inatoa sura halisi ya hali itakavyokuwa hadi kufika Jumatatu ambayo ndiyo mwisho.

Hakuna ubishi kuwa wapo waliokuwa na vitambulisho vya zamani na namba ambao walitakiwa kuvibadilisha, hivyo kuanza mchakato upya, lakini uhaba wa vifaa kwa Nida umekuwa changamoto kubwa.

Mathalani, katika kituo cha Kawe jijini Dar es Salaam, kuna msongamano mkubwa wa watu na vifaa vilivyopo kwenye kupiga picha na kuchukua alama ni vya watu watano pekee kwa wakati mmoja.

Iwapo wengi wataachwa bila kujiandikisha maana yake ni harasa kwa serikali, taasisi za fedha, kampuni za simu na mtu mmoja mmoja kwa kuwa hawataweza kufanya miamala kwa njia ya kielektroniki.

Kila dakika kuna miamala ya simu inayotumwa na kupokelewa na watumiaji ambao hutuma fedha kwa simu, simu kwenda benki, kutoka benki kwenda kwenye simu, kuhamisha akaunti moja kwenda nyingine, au kulipa malipo ya serikali.

Kote huko serikali inapata fedha ambazo ni kodi mbalimbali, sasa kwa watu milioni 22 kuachwa nje maana yake kuna hasara itakayopatikana kwa muda ambao watu watakuwa wanasubiri vitambulisho vya Taifa.

Kwa msingi huo, upo umuhimu wa kufanyika tathmini ya hadi Jumatatu kisha kufanya uamuzi wa kuongeza muda wa mwisho kwa Nida kuharakisha upatikanaji wa namba za utaifa ili watu wajisajili.

Kimsingi, hakuna tatizo kwenye kusajili laini kwa kuwa haichukui hata dakika tatu kukamilika, lakini tatizo lipo kwenye kupata namba za utaifa ambazo watu wanazisotea kuanzia asubuhi hadi jioni na bado hawafanikiwi.

Naamini mamlaka zikiwasiliana vizuri na kujiridhisha na taarifa za wahusika, wataweza kutoa namba haraka, ikiwamo kwa na mfumo wa kutuma ujumbe mfupi kwa wahusika ili waende wakachukue namba zao.

Faida za kiuchumi ni nyingi zaidi kwa kuwa athari zitajitokeza kwa watu binafsi, taasisi binafsi na serikali yenyewe kutokana na ukuaji wa kasi wa sekta ya fedha kwa njia yakielektroniki.

## HABARI KITAIFA



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa aliyekuwa Mbunge wa Newala Vijijini, Rashid Ajali Akbar, nyumbani kwake, Newala Mjini mkoani Mtwara jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Waethiopia 27 mbaroni tuhuma uhamiaji haramu

**Na Julieth Mkireri, BAGAMOYO**

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani limewakamata wahamiaji 27 raia wa Ethiopia kwa tuhuma za kuingia na kuishi nchini bila kibali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyogesa, alisema wahamiaji hao walikamatwa Januari 14 na 15 katika shughuli za kiopetesheni zinazofanywa na jeshi hilo.

Kamanda Wankyo alisema katika awamu ya kwanza wahamiaji haramu 11 walikamatwa Januari 14, katika maeneo ya Mlingotini Kata ya Zinga Wilaya ya Bagamoyo, ambao ni Pakatala Margus, Muratu Sawore, Yoseph Erose, Meimush Abise, Gazalose Samo.

Wengine ni Demere Deseign, Figure Dala, Merimum Alema, Jaraparu Mushahamo, Akilu Amari na Abidet Kahiru.

Kamanda Wankyo alisema Januari 15, Polisi wakiendelea na operesheni yao waliwakamata wahamiaji haramu wengine 16 katika eneo hilo la Mlingotini.

**Kamanda huyo wa Polisi alisema, katika mahojiano ya awali wahamiaji hao, wameonyesha wameingia nchini kwa kupitia bandari bubu ya Mlingotini kwa kutumia usafiri wa jahazi ambalo walilitelekeza ufukweni.**

Wankyo aliwataja wahamiaji hao ni Abdul Defulegn, Abdi Kairu, Akililu Tagel, Daniel Demak, Tarakgn Mshumo, Damere Detalegn, Gazahrgn Salu, Fikile Degul, Mamushi Adise, Merhun Alemaph, Takatal Markos, Mviatu Samore, Fiadu Erbiko, Akililu Amanael Daliso Osire na Yoseph Erose.

Kamanda huyo wa Polisi alisema, katika mahojiano ya awali wahamiaji hao, wameonyesha wameingia nchini kwa kupitia bandari bubu ya Mlingotini kwa kutumia usafiri wa jahazi ambalo walilitelekeza ufukweni.

Alisema, wahamiaji hao haramu lengo lao ni kwenda Afrika Kusini kutafuta maisha, na walikutwa ufukweni wakiwa kwenye harakati ya kutafuta usafiri kuendelea na safari yao.

Kamanda huyo alisema wahamiaji haramu hao watafikishwa Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Pwani kwa hatua za kisheria.

# TNBC kutumia bil. 1/- mapinduzi ya kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Biashara (TNBC) limesema katika kutekeleza mpango kazi wake katika nusu ya mwaka wa fedha wa 2019/2020 na kuchangia katika mapinduzi ya kiuchumi nchini, linatarajia kutumia shilingi 1,104,590,000.

Katika taarifa iliyotolewa jijini Dar es Salaam juu ya shughuli za baraza kwa mwaka wa fedha 2019/2020, baraza halikutoa mchanganuo wa kiasi cha fedha utakaochangwa na wadau, lakini limesema litapokea mgao wa serikali, mgao wa mradi wa LISC na mgao kutoka wadau wengine.

Taarifa hiyo kwa vyombo vya habari ilisema kwa kuwa TNBC inatazamiwa kuchangia vikubwa katika mapinduzi ya kiuchumi Tanzania, pamoja na mambo mengine, baraza linatarajia kushirikiana na Tamisemi kuhakikisha Mabaraza ya Mikoa na Wilaya yanakutana kama ilivyoainishwa kwenye mwongozo Ilifafanua kuwa itafanywa jitihada ya kuimarisha baraza na kuwa kitovu cha taarifa zinazohusu maboresho ya mazingira ya biashara, nchini na kuendelea kushirikiana na wadau katika kufanya tafiti zitakazochochea majadiliano yenye tija kati ya sekta ya umma na binafsi. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, TNBC itaanda ajenda za tafiti zinazohusu uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini; litapanua wigo wa majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

"Katika hili, baraza linatarajia kufanya majadiliano katika maeneo yafuatayo kadhaa ikiwamo ushiriki wa mwanamke katika uwekezaji na biashara ikiwemo changamoto zake; zinazokabili biashara ndogo ndogo, za kati na fursa zilizopo."

TNBC imesema inakusudia kutumia fedha hiyo katika kuendelea kuchochea ukuaji wa uchumi na mapinduzi ya viwanda nchini, kwa kuhakikisha mipango kazi ya vikundi kazi inatekelezwa kwa ufanisi na tathimini inafanywa kuangalia utekelezaji wake.

Pia kuandaa mkakati wa kuendeleza Sekta ya Misitu nchini ili iweze kuwa na mchango mkubwa kwenye pato la Taifa na utengenezaji wa ajira, kuandaa mapendekezo ya mkakati wa matumizi ya nishati kwa maendeleo ya viwanda nchini.

Kadhalika kuandaa mapendekezo ya maeneo ya ujuzi unaohitajika kwa ajili ya mapinduzi ya viwanda, kutoa mchango wa kitaalamu katika mapitio ya Sera ya Kilimo na Sera ya Misitu, kutathmini ushiriki wa sekta binafsi katika biashara za kimataifa ikiwamo biashara katika nchi za Junuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa

Afrika (SADC) na kuandaa mapendekezo ya maeneo ya kimkakati yenye fursa za ushirikiano kati ya biashara ndogo, za kati na kubwa.

Baraza limesema linaamini hatua hii itahakikisha jamii kubwa ya Watanzania wanafaidika na mapinduzi ya kiuchumi nchini.

Kadhalika, baraza litaandaa mikakati ya kuhamasisha matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji miongoni mwa Watanzania na kusema kwamba hatua hii itasaidia kuongeza tija katika matumizi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Baraza pia limesema litaendelea kuimarisha ushirikiano uliopo katika ya sekta binafsi na umma katika kuchochea mapinduzi ya kiuchumi nchini.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **ADILI AUCTION MART COMPANY LIMITED, JAGA AUCTION MART, WAUNGWANA AUCTION MART na KOTI BROTHERS** kwa niaba ya AccessBank Tanzania Limited watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Magari na Viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA WENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | LUMUMBA | JAGA AUCTION MART | LIKOKOLA/MADI,YOLUU | LIKOKOLA/MADI,YOLUU | TOYOTA RAUM T 128 DFX | TABATA | 24/01/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 2 | LUMUMBA | ADILI AUCTION MART | KAAYA/SAMWEL,ESTER | KAAYA/SAMWEL,ESTER | HOUSE | MBEZI | 15/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 3 | MBEYA | KOTI BROTHERS AUCTION MART | NDIMBO/A,AMBROSE | NDIMBO/A,AMBOSE | HOUSE | MLOWO-MBOZI | 01/02/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 4 | LUMUMBA | ADILI AUCTION MART | DANJI/JAYANT,MANISH | DANJI/JAYANT,MANISH | TRAILER T172AMT | MTONI KIJICHI | 25/01/2020 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 5 | LUMUMBA | WAUNGWANA | KIRIA/M,DAMAS | CHUWA/J,DAMAS | IST T201 DPN | TABATA | 24/01/2020 SAA 4:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**ADILI AUCTION MART COMPANY LIMITED 0753077885**
**JAGA AUCTION MART 0713123427**
**KOTI BROTHERS 0713235517**
**WOTE MNAKARIBISHWA.**

215588402



Wananchi wakijiandaa kuuaga mwili wa Daudi Jilala (24) jana, anayedaiwa kuuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani nyumbani kwake Mtaa wa Mabambase, Manispaa ya Shinyanga, na baadaye kusafirishwa kwenda Kijiji cha Mwabagalu Malya, wilayani Maswa kwa ajili ya maziko. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Akutwa amekufa siku 3 chumbani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

DAUDI Jilala (24), mkazi wa Kijiji cha Mwabagalu Malya, wilayani Maswa mkoani Simiyu, aliyekuwa akifanya biashara ya kusafirisha abiria kwa kutumia baiskeli, amekutwa akiwa amekufa chumbani kwake siku tatu katika Mtaa wa Mabambase, Kata ya Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga. Imedaiwa kuwa kijana huyo alikutwa na umauti baada ya kupigwa na kitu kizito kichwani.

Akisimulia tukio hilo jana, jirani na marehemu, Jesca Simoni, alidai kuwa Jumapili alipoamka kwenda kwenye shughuli zake za utafutaji, aliona mlango wa kijana huyo ukiwa umefungwa kwa kufuri na aliporudi aliukuta vilele hadi juzi ndipo akaona chumba kipo wazi huku kikitoa harufu kali. Alidai baada ya kubaini harufu kali ikitoka ndani ya chumba hicho, akahisi huenda ni choo, lakini akawa anaona inzi wakitoka ndani ya chumba hicho, ndipo akamwambia rafiki yake wachungulie ndipo wakaona kuna kitu kimevimba kitandani kikitoa harufu kali na kuamua kukimbilia kwa majirani kutoa taarifa.

Alidai baada ya kutoa taarifa kwa majirani, walimjulisha Mwenyekiti wa Mtaa, walikwenda kuangalia kilichoko kwenye chumba hicho na walipofanya ukaguzi waliukuta mwili wa kijana huyo ukiwa na majeraha kichwani.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Bakari Simoni, alikiri kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa kijana huyo inasemekana siku za hivi karibuni alikuwa akiishi na mwezake ambaye alimkaribisha, na baada ya kutokea tukio hilo mwezake huyo hajaonekana tena na hajulikani aliko.

Alisema baada ya kupewa taarifa juu ya tukio hilo na jirani yake, alitoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ambalo nalo lilifika eneo la tukio likiwa na daktari, na baada ya kufanya uchunguzi, walitoa taarifa kuwa ameuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani. Mjomba wa marehemu, Paulo Shishi, alisema kuwa baada ya kupewa taarifa juu ya tukio hilo walifunga safari kwenda Shinyanga Mjini, ili kuchukua mwili wa mpwa wake kwa ajili ya mazishi ingawa awali ilikuwa imepanga uzikwe Shinyanga kwenye makaburi ya Dodoma.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Joseph Paulo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, na kubainisha kuwa Jeshi la Polisi linafanya uchuguzi juu ya tukio hilo ili kumbaini mhusika wa mauaji hayo.

# Umuhimu uchangiaji damu waelezwa

**Na Mary Geofrey**

WATANZANIA wametakiwa kujitokeza kuchangia damu wakati wowote badala ya kusubiri majanga yatokee, kwa ajili ya kusaidia makundi ya watu wanaohitaji huduma hiyo kwa wingi ambao ni majeruhi wa ajali, wajawazito, watoto na wagonjwa wa saratani.

Rai hiyo ilitolewa na Meneja wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama, Dk. Magdalena Lyimo, wakati akizungumza na maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, wakati wa ziara ya kampeni ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya' kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais John Magufuli.

Alisema Watanzania wengi wanapenda kujitokeza kuchangia damu wakati yanapotokea majanga mbalimbali kama ajali za barabarani na moto.

Alitolea mfano wa tukio la ajali ya moto ililotokea eneo la Msavu mkoani Morogoro Agosti 10, mwaka jana na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 100, katika kipindi cha muda mfupi walikusanya chupa 2,328 za damu kutoka mikoa mbalimbali nchini.

"Wito wetu kwa jamii ni kuendelea kujitokeza kuchangia damu kwa wingi kwa ajili ya kusaidia wenzetu wanaopata majanga ya ajali ili kuokoa maisha yao.

Kwa kipindi ilipotokea ajali ya lori la mafuta mkoani Morogoro mwaka jana, jumla ya watu 2,328 walio-jitokeza kuchangia damu kwa ajili ya kusaidia majeruhi kutoka maeneo mbalimbali nchini," alisema Dk. Lyimo. Alisema kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Magufuli, wamefanikiwa kuongeza ukusanyaji wa damu kutoka asilimia 40 mwaka 2016/17 hadi asilimia 60 mwaka 2018/19.

Alisema kwa mwaka wanakusanya chupa za damu 390,379 kwa takwimu za mwaka 2018/19 kutoka chupa 257,557 mwaka 2017/18 wakati lengo likiwa ni kukusanya chupa 500,000 kwa mwaka sawa na asilimia 100 ya mahitaji yote. Alisema kwa mwezi wanakusanya damu kutoka kwenye vituo vyao vilivyopo kote nchini chupa 25,000 hadi 30,000.

Kadhalika alisema wameboresha utendaji kazi kutokana na serikali kununua mashine za kisasa za upimaji mpya 24 zilizosambazwa katika kanda sita za ofisi zao.

Alisema mashine hizo zilizonunuliwa kwa gharama ya Sh. bilioni 13.248 na zina uwezo wa kupima homa ya ini B na C, kaswende na maambukizi ya Ukimwi kwa wakati mmoja.

# Wanaouza maziwa yenye maji kukiona

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama mkoani Shinyanga imesema itawachukulia hatua za kisheria kwa kuwafikisha mahakamani wauza maziwa wote ambao wamekuwa na tabia ya kuuza maziwa yaliyochanganywa na maji.

Maziwa hayo yanasadikika kuwa sio safi na salama. Angalizo hilo lilitolewa jana na Katibu Tarafa ya Kahama, Julius Chagama, katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri ya Mji wa Kahama cha robo ya pili ya mwaka wa fedha Oktoba hadi Desemba mwaka 2019. Alisema wafanyabiashara wa maziwa wamekuwa na tabia ya kuchanganya maziwa na maji yanayosadikika sio safi na salama na kuyauza mbele ya Hospitali ya Mji wa Kahama na kuwauzia wagonjwa.

"Ofisi ya Mkuu wa wilaya kwa kushirikiana na wataalamu wa afya tumeanza mchakato wa kuwasaka wauza maziwa wote ambao wamekuwa na tabia ya kuchanganya maji na maziwa, na atakayebainika atakuwa mfano kwa wauza maziwa wote," alisema Chagama.

Chagama alisema ni bora maziwa yakauzwa kwa bei kubwa yakiwa na virutubisho vyote vinavyotakiwa kuliko kuuza maziwa kwa bei ndogo yakiwa yamechanganywa na maji, ambayo haijulikani yamechotwa wapi.

Aidha, Chagama alisema, katika ufuatiliaji waliofanya na wataalamu wa afya, imebainika maziwa mazuri yanatoka Mkoa wa Kagera na maeneo ya Ngara na Nyakanazi, huku maziwa yanayotoka wilayani Kahama na wilaya za jirani yakiwa yametiwa maji mengi.

Pia aliwataka madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Kahama kushirikiana na wataalamu wa afya kwenye kata zao kuwabaini wauza maziwa wote wanaochanganya maji na maziwa hasa kwenye hoteli ili waweze kuchukulia hatua za kisheria. Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, alisema kuwa kiwanda cha maziwa cha Kagongwa kinashindwa kujiendesha vile inavyotakiwa baada ya kukosekana kwa maziwa ya uhakika.

Alisema kiwanda hicho kina uwezo wa kuchakata maziwa safi lita 3,000 kwa siku na kwa wakati mmoja lita 500, na kuwataka wafugaji wa ng'ombe kufugia ndani na kuitafutia chakula pamoja na kukamua maziwa na kwenda kuuza kwenye kiwanda hicho.

HABARI KITAIFA

# Bosi Takukuru: Waliotafuna fedha za korosho kuzitapika

**Na Futuna Seleman,** RUFIJI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) imesema itapiga kambi wilayani Rufiji mkoani Pwani kuhakikisha watu wote waliohusika katika kuchukua fedha za wakulima wa korosho wanazirejeshwa na walengwa wanapata haki yao.

Imesema itapita nyumba hadi nyumba kuwasaka watuhumiwa watakaobainika kuchukua fedha hizo kazi itakayoanza Februari mosi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbungo, ndiye aliyetoa maagizo hayo akiwa Rufiji wakati akizungumza na wakulima wa korosho wanaolalamikia malipo ya fedha zao za korosho ya mwaka 2018/2019/2020.

"Mimi niwatoe hofu hizi fedha zitalipwa, hakuna mtu ambaye hatarejeshewa hizi fedha, katika hili itachukua muda kidogo, lakini fedha zitalipwa kama tumefanikiwa Lindi ambako wakulima walikuwa wanadai bilioni moja," alisema na kuendelea:

"Ni fedha nyingi sana zimelipwa, hapa nimeambiwa mnadai Sh. milioni 34 hizo ni pesa ndogo sana zitalipwa, mimi niwaahidi nitaleta timu yangu kwa kushirikiana na ofisi ya mkuu wa wilaya na Takukuru tutatengeneza kambi hapa watapita nyumba hadi nyumba mlango hadi mlango kwa mtu ambaye tutakuwa na ushahidi kuwa amechukua pesa atazitapika."

"Niwatoe wasiwasi na shaka watu mmeongea kwa uchungu na inatia uchungu kwamba kulima mwaka mzima ametumia nguvu zake kukaa shambani kulima kuchomwa miba ametumia fedha zake za akiba kupalilia halafu leo watu wachache wasiozidi hawazidi watano kutoka chama cha msingi anachukua tu zile fedha kiulaini... haiwezekani, hao watu watazitapika tu toeni ushirikiano hao watu ni nani? Watazirejesha tu."

Akijibu nalalamiko na baadhi za wakulima kuwa taasisi hiyo haifanyi kazi ipasavyo na ndio chanzo cha wao kudhulumiwa fedha zao, Brigedia Jenerali Mbungo alisema kuwa lawama hazijengi bali zinabomoa kwa sababu rushwa inafanywa katika jamii inayotuzunguka.

"Rushwa ipo sehemu zozote, mahali popote mmenielewa ndugu zangu?" Alihoji na kuendelea:

"Udhaifu wa mtu mmoja usiichafue taasisi yote, kazi mnayotakiwa kuifanya ni kuripoti makao makuu au nipigieni mwenyewe."

Alisifu jitihada zilizofanywa na serikali na Wilaya ya Rufiji kwa kushirikiana na Takukuru kuhakikisha Sh. milioni 90 za wakulima wa korosho zilizoyeyuka zimepatikana.

Hamza Said aliilalamikia Takukuru wilaya kuwa imeshindwa kuwasaidia wakulima hadi sasa na ndio maana wanahangaika wakiwamo wazee.

Mussa Mng'eresa alisema ubabaishaji wa baadhi ya viongozi wa vyama vya msingi kushindwa kuelewa vema maagizo ya awali ya serikali yamepelekea hali hiyo kwa kuwa baadhi walitaka kutajirika kupitia fedha za wakulima wanyonge.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Juma Njwayo, alisema serikali imechukua hatua madhubuti kufuatilia fedha za wakulima wa korosho kwa baadhi ya vyama vya msingi zilizochukuliwa.



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku (kushoto), akizungumza wakati wa warsha ya wadau wa vyombo vya habari na waandishi wa habari kuhusu ujenzi wa nchi ya amani kuelekea katika uchaguzi mkuu Oktoba mwaka huu, iliyoandaliwa na taasisi hiyo, jijini Arusha jana. Katikati ni Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, David Eliamongi na Msaidizi Maalum wa Taasisi hiyo, Galus Abeid. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Vibali uagizaji dawa vyaongezeka

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Chakula na Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imeongeza idadi ya vibali vya uingizaji na utoaji wa bidhaa nje ya nchi kutoka vibali 13,018 kwa mwaka 2015/16 hadi vibali 26,478 mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 203.

Imeelezwa kuwa mafanikio hayo yametokana na kuwapo kwa mfumo wa kielektroniki wa utoaji vibali vya kuingiza na kutoa bidhaa nchini, unaowezesha wateja kutuma maombi na kufanya malipo popote walipo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, aliyasema hayo katika ofisi za mamlaka hiyo jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na maofisa mawasiliano kutoka katika taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto katika ziara ya kampeni yao ya 'Tumeboresha Sekta ya Afya'.

"Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano, TMDA ambayo awali ilikuwa TFDA, tumefanikiwa kuboresha huduma hasa za utoaji wa vibali baada ya kuwa na mfumo huu mpya unaotoa huduma kisasa," alisifu.

Alisema mamlaka hiyo pia imefanikiwa kupunguza idadi ya bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba visivyofaa kwa matumizi ya binadamu, baada ya kuboresha utendaji kazi, kutoka tani 140,705 mwaka 2017/18 zilizokuwa na thamani ya Sh. milioni 22.394 hadi kufika tani 664 mwaka 2018/19.

"Hii inaashiria kupungua kwa bidhaa zisizokidhi viwango katika soko la Tanzania kutokana na kazi kubwa inayofanywa na mamlaka za kudhibiti uaingizaji," alifafanua.

Alisema wanadhibiti, kuondoa na kuteketeza bidhaa ambazo hazikidhi vigezo vya ubora, usalama na ufanisi ili kuepusha zisitumiwe na walaji.

Alisema kufuatia mpango wa ufuatiliaji wa ubora wa bidhaa katika soko, sampuli 1,136 za dawa za binadamu zilifuatiliwa na kuchunguzwa katika kipindi cha miaka minne na asilimia 96 ziliendelea kukidhi vigezo vya ubora.

Alieleza kuwa kati ya sampuli 144 za dawa za mifugo zilizochunguzwa katika kipindi hicho, asilimia 90 zinaendelea kukidhi vigezo vya ubora.

Fimbo alisema mamlaka pia imeweka mifumo madhubuti ya ufuatiliaji wa madhara yatokanayo na matumizi ya dawa na vifaa tiba ili kutambua, kutathmini na kuzuia madhara yasiyovumilika yasitokee kwa wananchi.

Alisema ili kuimarisha upatikanaji wa taarifa hizo, TMDA imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya dawa kwa kutumia simu ya mkononi au kompyuta na njia ya kutuma ujumbe wa simu.

Kuhusu mipango na malengo ya TMDA, alisema wanalenga kujenga maabara kubwa na ya kisasa ofisi za makao makuu za jijini Dar es Salaam na Dodoma ili kuboresha utendaji kazi wa mamlaka hiyo.

Alisema jengo lake litakuwa la ghorofa saba likiwa na maabara kubwa na ya kisasa, vifaa tiba, vitendanishi na vifaa vya kutosha.

# Madiwani walia na miradi viporo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, limejadili makadirio ya bajeti ya mwaka (2020-21) ya Sh. bilioni 39, na kuazimia bajeti hiyo ilenge zaidi kukamilisha miradi viporo.

Hayo yalibainishwa juzi na madiwani wa halmashauri hiyo kwenye kikao cha Baraza la Bajeti, baada ya Ofisa Mipango wa Halmashauri, Imelda Kirima, kumaliza kuwasilisha makadirio ya bajeti ya halmashauri.

Madiwani hao walisema ni vyema fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye bajeti hiyo ikaelekezwa kwenye ukamilishwaji wa miradi viporo, ambayo ilijengwa kwa miaka mingi na haijakamilika, ili ianze kufanya kazi ya kuhudumia wananchi kuliko kuibua miradi mipya.

Nicodemas Simoni wa Kata ya Masengwa, alisema kuna miradi mingi ya ujenzi ambayo imejengwa kwa nguvu za wananchi na kufikia usawa wa renta, lakini bado hajikamilika, hivyo ni vyema miradi hiyo ikamilishwe kwanza ili itoe huduma kwa wananchi, kuliko kuibua miradi mipya.

"Mfano kwenye Kata ya Masengwa kuna maboma mawili, moja ni zahanati, na jingine ni nyumba ya walimu, yamejengwa kwa miaka mingi hadi kufikia usawa wa renta, lakini mpaka sasa hayajakamilika, hivyo kushindwa kutoa huduma...hivyo napendekeza bajeti hii ikamilishe kwanza miradi viporo," alisema Simoni.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ngassa Mboje, aliwasihi madiwani hao kuipitia vizuri bajeti hiyo, ili kwenye upungufu pafanyiwe marekebisho, na kubainisha bajeti hiyo italenga zaidi kukamilisha miradi viporo iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

Ofisa Mipango Kirima, akiwasilisha makadirio ya bajeti ya mwaka 2020-21, alisema ni Sh. 39,009,580.226, na kwamba mishahara imetengewa Sh. 29,901,156,000 wakati fedha za miradi ya maendeleo ni Sh. 6,993,706,159.

HABARI KITAIFA

# Kabudi awapa somo wahitimu Diplomasia

**Na Enock Charles**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Prof. Palamagamba Kabudi, amewataka wahitimu wa Chuo cha Diplomasia kutumia maarifa waliyoyapata chuoni hapo kujiajiri au kutafuta ajira katika sekta binafsi aliyosema ni kubwa zaidi kuliko kutegemea fursa za ajira serikalini.

Akizungumza katika mahafali ya 22 ya chuo hicho, Prof. Kabudi alisema kwa sasa serikali ipo katika kipindi cha kuboresha viwanda vya aina mbalimbali ambavyo hapo baadaye vinatarajiwa kutoa ajira kwa wananchi kama mojawapo ya mikakati ya serikali katika kupunguza tatizo la ajira nchini na kukuza uchumi wa nchi.

"Nafahamu wengi wenu mnaweza kuwa na mawazo kwamba mgeni rasmi ambaye ni waziri mwenye dhamana tena ya mambo mliyosomea anaweza kusema chochote kuhusu ajira, wito wangu kwenu ni kwamba serikali inaendelea kuongeza wigo wa ajira katika sekta za umma na za binafsi, ikumbukwe pia kwamba azima ya serikali ya kuanzisha sera ya viwanda ni sehemu ya mikakati ya kuongeza ajira," alisema Prof. Kabudi.

Huku akinukuu maneno ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Prof. Kabudi, alisema elimu sio njia ya kuepuka umaskini bali ni nyenzo ya kukabiliana nao, akiwataka wahitimu hao kutumia maarifa waliyoyapata chuoni kukabiliana na tatizo la umaskini badala ya kusubiri ajira kutoka serikali ambayo haiwezi kuajiri wahitimu wote.

Prof. Kabudi alitoa rai kwa chuo hicho kuangalia uwezekano wa kuanzisha kozi za ujasiriamali ili kuwafundisha wanafunzi stadi mbalimbali za ujasiriamali katika kuhakikisha kuwa wasomi wanaohitimu hapo wanapata ujuzi utakaowawezesha kukabiliana na umaskini baada ya kumaliza masomo yao na kuagiza kuwa masomo hayo yafundishwe kwa lazima.

Akizungumzia kuhusu programu mpya zilizoanzishwa chuoni hapo, alitaka kuboreshwa kwa mafunzo ya Diplomasia kuhusu usalama na mitandao kutokana na tahadhari iliyopo duniani kuhusu tishio la ugaidi katika nchi za Afrika.



Rundo la takataka zikiwa zimetelekezwa kwa muda mrefu jirani na eneo la maegesho ya Bajaji katika stendi ya Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachosababisha kero na harufu mbaya kwa madereva. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Standard Chartered yazindua malipo kwa njia ya mtandao

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Standard Chartered, imezindua mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao ujulikanao kama 'Straight2Bank-NextGen', utakaowawezesha wananchi kulipia huduma mbalimbali zikiwamo za serikali.

Akizungumza kuhusu huduma hiyo jana jijini Dodoma, Mtaalamu wa Huduma za Benki Mtandao na Malipo ya Serikali Mtandao, Mwiga Kapya, alisema huduma hiyo itawezesha mtumaji na mpokeaji kupata taarifa ya papo hapo pindi muamala wa malipo unapofanyika.

"Pia, mtumaji wa fedha atapokea stakabadhi ya malipo papo hapo kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu ya malipo yake kwa baadaye," alisifu. Alisema huduma hiyo inawarahishia wateja kutokukosea wakati wakifanya malipo yao, akibainisha kuwa mwananchi yeyote anaweza kuitumia.

"Benki ya Standard Chartered inaendelea kuboresha huduma zake za dijitali ili kuwasaidia wananchi na wafanyabishara wakati wakifanya malipo yao hususani malipo ya kodi, tutaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali za serikali," alitamba.

Mkurugenzi wa Mifumo ya Fedha na Mipango, John Sausi, aliipongeza Benki ya Standard Charted kwa kuanzisha mfumo huo ambao unawahusu wanananchi wote hata wasiotumia huduma za kibenki.

# Wizara kuboresha masoko ya samaki

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imeanza mpango kabambe wa kufufua, kujenga na kukarabati mialo na masoko yote ya samaki nchini kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa ajili ya kuhudumia soko la ndani na nje ya nchi.

Mpango huo wa uboreshaji wa mazingira hayo ya shughuli za uvuvi yameanzia kwenye Soko la Kimataifa la Samaki la Magogoni Feri jijini Dar es Salaam, serikali iktenga takribani Sh. bilioni mbili kulifanyia ukarabati mkubwa wa miundombinu yake na kupanua wigo mpana zaidi wa biashara za kimataifa.

Wizara hiyo pia imeingia mkataba na Mshauri Mwelekezi M/S Inter Consult Ltd kwa ajili ya kutayarisha michoro na makadirio ya ukarabati wa soko hilo na imeshampata mzabuni kwa ajili ya ukarabati wa soko hilo na kazi hiyo itaanza hivi karibuni.

Akitangaza mpango huo wa uboreshaji wa mialo na masoko ya samaki kote nchini sambamba na kukabidhi vyoo vipya vya kisasa vyenye matundu 12 vilivyojengwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Manispaa ya Ilala Dar es Salaam, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alisema serikali imekataa wavuvi na shughuli za uvuvi kudharauliwa.

Waziri Mpina alisema jengo hilo jipya lililojengwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, lina uwezo wa kuhudumia watu 40 kwa wakati mmoja, hivyo kukamilika kwa vyoo hicho ni hatua madhubuti ya kuboresha afya za watumiaji wa soko hilo wakiwamo wavuvi, wachakataji wa samaki, mama lishe, wanunuzi wa samaki na wadau wengine.

Waziri Mpina alisisitiza kuwa kwa miaka mingi sasa wavuvi na shughuli za uvuvi wamekuwa wakidharauliwa na kutopewa msukumo wowote na kwamba serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli imekuja kuwafuta machozi.

Alitoa miezi mitatu kwa halmashauri zote kuboresha mialo na masoko yote nchini na kueleza kusikitishwa kwake na tabia iliyojengeka ya baadhi ya halmashauri kugeuza mialo na masoko kuwa chanzo cha mapato ya halmashauri na kushindwa kuboresha miundombinu yake, hasa vyoo na kutotekeleza Sheria za Uvuvi Namba 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009

Mpina alisema wizara imekamilisha kazi ya ujenzi na kukabidhi kwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, akimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wake kuhakikisha mradi huo unasimamiwa, kutunzwa na kutumika kama ilivyokusudiwa.

Pia alimwagiza Katibu Mkuu (Uvuvi) kuandaa na kusambaza miongozo ya usimamizi wa masoko na mialo kwa wadau na halmashauri zote nchini ifikapo Februari Mosi, mwaka huu, ili kuweka masharti ya uendeshaji na usimamizi makini wa shughuli za uvuvi.

Aliipongeza menejimenti ya soko hilo kwa hatua ya kupunguza matumizi kutoka Sh. milioni 100 hadi kufikia milioni 73 kwa mwezi tangu walipopokea maelekezo yake aliyoyatoa mwaka jana.

Katibu Mkuu, Rashid Tamatamah, alisema mradi wa vyoo hivyo umegharimu Sh. milioni 163 na kwamba utapunguza adha kwa wananchi wanaotumia soko hilo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala, Charangwa Makwiro, alimshukuru Waziri Mpina kwa uamuzi wa wizara kujenga vyoo hivyo na kuhakikishia kuwa kama serikali ya wilaya itasimamia miundombinu hiyo ili idumu kwa miaka mingi.

# Serikali yaomba ratiba maonyesho China

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SERIKALI imeuomba ubalozi wa China kuipatia ratiba za maonyesho ya madini nchini kwao ili wafanyabiashara wakubwa wa madini nchini washiriki ili kutangaza aina za madini yaliyopo nchini.

Ombi hilo lilitolewa jana jijini hapa na Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, wakati akifunga mkutano wa mabalozi wa China na Tanzania pamoja na wafanyabiashara wa madini ulioandaliwa na Chama cha Wafanyabiashara Wakubwa wa Madini (Tamida).

Naibu Waziri Nyongo alisema wakipata ratiba za maonyesho hayo, itakuwa fursa nzuri kwa wafanyabiashara nchini kutangaza madini yaliopo ambayo mengi hayajulikani japo ni mazuri na ya kipekee.

"Na nyie wafanyabiashara mkipata fursa hiyo tumieni vizuri pamoja na kutafuta soko la uhakika la madini yetu kwa sababu China kuna soko kubwa la madini," alisema.

Pia aliagiza wafanyabiashara wakubwa wa madini nchini walioko kwenye soko la madini mjini Arusha, kuzipandisha hadhi ofisi zao ili kuvutia watalii wengi kuwatembelea na kununua madini yao.

"Ikiwezekana angalieni ofisi jengo la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), ili ziwe na hadhi ya kuvutia. Watalii wakija hapa watembelee hapo kununua zawadi za kwao," alisema Nyongo.

Alisema kwa kuboresha ofisi kutasaidia kupata fedha za watalii ambazo huishia hotelini na kurudi kwao.

Naye Balozi wa China nchini, Wang Ke, aliahidi kutoa ratiba za maonyesho hayo ili wafanyabiashara wapate fursa za kupata soko la madini.

Alisema China wanatumia sana madini katika vitu mbalimbali, hivyo ni sehemu muhimu kwa soko la uhakika la madini.



Balozi wa China nchini, Wang Ke, akiwa ameshika madini ya tanzanite, huku akipata maelezo kutoka kwa Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania (TAMIDA), Sam Mollel (wa pili kushoto), alipotembelea maonyesho kabla ya mkutano wa balozi huyo na wa Tanzania nchini China na wafanyabiashara wa madini, jijini Arusha juzi. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Ubakaji, ulawiti watoto vyashamiri Hanang'

**Na Jaliwason Jasson,**
HANANG'

HALMASHAURI ya Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara imesema watoto 24 wamebakwa na wawili kulawitiwa kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya hiyo, Martha Sulle, alisema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe juu ya hali ya ulinzi na usalama wa watoto.

Sulle alisema watoto hao walibakwa Oktoba hadi Desemba, mwaka jana na kufanya vitendo vya kinyama viendelee kushika kasi wilayani hapa.

Alizitaja sababu zinazofanya matukio hayo kuwapo kwa watoto hasa wa miaka sifuri hadi minane kuwa ni familia nyingi kutelekeza watoto kwa walevi na watoto kutembea umbali mrefu kwenda shuleni.

"Wafugaji kuhamisha ng'ombe na nyumbani kuacha wachungaji pekee, kunahatarisha usalama wa watoto. Wachungaji wanaoachiwa watoto ndio wanawabaka na kuwalawiti kwa sababu ya kukosa ulinzi," alisema.

Aidha, alisema makundi yanayoongoza kwa kubaka na kulawiti ni vijana wa kuanzia miaka 17 hadi 40 na kundi lingine ni baadhi ya wazee.

"Mengine yanayosababisha ubakaji huu ni imani za kishirikina. Mfano mtu anabaka na kulawiti kwa wakati mmoja na wengine wanawakomoa watoto baada ya familia kuwa na ugomvi," alisema Sulle.

Katika kuhakikisha wilaya inatokomeza ubakaji wa watoto hao, alisema watahakikisha kila anayehusika na matukio hayo anachukuliwa hatua za kisheria.

"Katika kipindi cha Oktoba na Novemba, mwaka jana, kesi mbili zilihukumiwa na wahusika kila mtu alihukumiwa kifungo cha miaka 30 jela," alisema.

Alisema mpaka sasa kesi zilizoko mahakamani za ulawiti ni kesi tatu na kesi za ubakaji tisa na zote za Oktoba hadi Desemba, mwaka jana.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Kituo cha Sheria Haki za Binadamu (LHRC) ya mwaka 2018 iliyotolewa Septemba Mosi, mwaka jana, watoto 2,365 nchini walibakwa.

Ripoti hiyo inasema katika kipindi cha miezi sita ya kwanza kwa mwaka huo, matukio ya ukatili wa watoto yaliyoripotiwa ni 6,376 wakati huo ya ubakaji yakiwa 2365.

# Wanafunzi kunufaika na taasisi za China

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BALOZI wa China nchini, Wang Ke, ameahidi kuwaunganisha wanafunzi wa Chuo cha Uhasibu Arusha na taasisi mbalimbali za biashara nchini China, ili wapate uelewa wa kukuza na kuendeleza biashara zao.

Aliyasema hayo jana jijini Arusha alipotembelea chuo hicho na kujionea kituo cha kukuza mawazo ya biashara yanayozalishwa na wanafunzi hao.

"Tukiwaunganisha na taasisi zetu China mtapata uelewa na ujuzi wa kukuza biashara zenu," alisema.

Balozi Wang alisema chuo hicho kinafanya vizuri kuwaandaa vijana hao kujiajiri kwa kuwaandaa kuwa na mawazo ya biashara yanayoendelezwa chuoni hapo na kuunganishwa na wadau pamoja na taasisi mbalimbali.


Alisema watahakikisha wanaendeleza ushirikiano wa kimasomo kati ya wanafunzi wa chuo hicho na hata walimu kwa kuandaa utaratibu wa kutembeleana ili kubadilisha uzoefu namna ya ufanyaji biashara kati ya nchi hizo mbili.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema chuo hicho kina jukumu la kukumbusha vijana kujitambua katika kutimiza wajibu wao ambapo uwepo wa kituo hicho cha kukuza biashara kwa vijana hao, kimeleta manufaa makubwa kwao.

Prof. Sedoyeka alisema wamekuwa wakitoa mafunzo kwa vijana hao na kuwaunganisha na masoko na vyanzo vya mitaji ili kukuza biashara zao.

Alisema kuwa wataendelea kukuza ushirikiano kati yao na watu wa China katika kushirikiana kwa pamoja kukuza mawazo ya biashara ya vijana hao na hata walimu kupata uzoefu zaidi ili vijana hao wajiajiri na kutoa ajira kwa wenzao. "Kituo hiki ni kipya bado na kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ukosefu wa vitendea kazi, pamoja na uelewa mdogo kuhusu masuala ya biashara, hivyo ushirikiano huu ni mzuri kwani utatuunganisha na wenzetu wa China na kuweza kujifunza masuala mbalimbali ya biashara na namna ya kuziboresha," alisema.

Mkuu wa Mkoa Arusha, Mrisho Gambo, alisema ujio wa balozi huyo umeleta manufaa makubwa kwa chuo hicho kwa kuongeza fursa za biashara kwa wanafunzi na walimu. Alikitaka chuo kutumia fursa hiyo ya upendeleo na watu wa China katika kuboresha na kuimarisha fursa za kibiashara kwa kuwasaidia wanafunzi na walimu ili kuzalisha biashara bora zaidi.





# Wahamasishwa uchimbaji wa madini 'gypsum'

**Na Mary Mosha,** SAME

SERIKALI wilayani Same katika kutekeleza agizo la sera ya viwanda na kuelekea uchumi wa kati, limewataka wananchi kujikita katika kuendelea kuchukua leseni na kuanza kuchimba madini ya gypsum badala ya kusubiri wawekezaji kutoka nje.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, aliiambia Nipashe kuwa kwa sasa wilaya hiyo inatafuta wawekezaji na sio lazima kusubiri wawekezaji kutoka nje na badala yake wazawa wanaweza kujichukulia leseni na kuanza kuchimba madini na kujiongezea kipato.

Senyamule alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na wanahabari juu ya namna bora ya kuwasaidia wawekezaji wa ndani kunufaika na rasilimali za ndani ambapo alisema kuwa imebainika gypsum inayopatikana Wilaya ya Same kwa kiwango kikubwa na yenye ubora wa hali ya juu.

Alisema wawekezaji wazawa wa wilaya hiyo wanapaswa kuongeza kasi ya kuomba leseni za madini zitakazowaruhusu kuchimba gypsum na kuondokana na tatizo la ajira ambalo limekuwa tatizo kwa vijana wengi.

"Tunatambua kuwa vijana wamekuwa wakilalamika kwa kukosa ajira sasa vijana wa wilaya yetu, neema imekuja hivyo tunapaswa kuichangamkia kwa kuomba leseni za madini na kuanza kunufaika na uchimbaji wa gypsum," alisema Senyamule.

Aidha, mkuu huyo wa wilaya aliuagiza uongozi wa kata hiyo kushirikiana kutenga eneo lenye madini hayo kwa ajili ya vijana hali itakayopunguza tatizo la ajira.

Senyamule alisema atakaa na idara ya madini ili kwenda kuwapa elimu wananchi juu ya taratibu za kupata leseni za uchimbaji lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa hawacheleweshwi katika kupata leseni hiyo.

Mmoja wa wananchi, Edwin Mvungi, alisema ikiwa serikali itapungunza urasimu katika utoaji wa taarifa, wawekezaji wa ndani wataweza kuwekeza katika uchimbaji wa madini.

"Ikiwa halmashauri ya wilaya itafuata mwongozo wa uwekezaji kwa kupunguza urasimu, na kujikita katika kutafuta wawekezaji, pamoja na kuwakusanya watu wenye vikundi vidogo, wataweza kufikia lengo kwa wakati," alisema Fransinc Mkwizu.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi na Ajira, Jenista Mhagama (katikati), akitoa maelekezo kwa watendaji mbalimbali wakiwamo makamanda waandamizi wa Jeshi la Magereza nchini, wakati wa ziara yake ya kukagua ujenzi wa mradi wa Kiwanda cha Ngozi cha Karanga kinachojengwa kwa ubia kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Gereza la Karanga, mjini Moshi. juzi. **PICHA: MAELEZO**

# Wakosoa mfumo vifurushi bima afya

**Na Mary Mosha,** MOSHI

BAADHI ya wakazi wa Mkoa wa Kilimanjaro wamesema mbali na elimu ya vifurushi vya bima ya afya kuendelea kutolewa, lakini bado kuna changamoto ya upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi kutoka vituo vya kutolea huduma hasa wenye kadi ya Mfumo wa Bima ya Afya (NHIF).

Wakizungunza katika uzinduzi wa vifurushi hivyo jana mkoani Kilimanjaro, Edward Mushi aliuomba uongozi huo kufanya mawasiliano na vituo vinavyotoa huduma za afya kuboresha huduma hizo ili kuwavutia wananchi wengi zaidi.

"Mfano Hospitali ya Rufani ya Mkoa Mawenzi, imebandikwa tangazo kabisa mwisho wa huduma kwa wenye bima ni saa tisa na nusu na mwishoni mwa wiki mwisho ni saa saba mchana, kutokana na hali hiyo hatuoni umuhimu wa kukata bima hiyo," alisema Aisha Mohamed na kuendelea: "Sasa changamoto kama hizo NHIF lazima mzichukulie hatua ili kujenga imani kwa Watanzania." Akizindua mpango huo wenye kauli mbiu 'Tumekusikia Jipimie' Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, aliitaka NHIF kujitafakari katika kutoa huduma bora kwa wanachama ili kukuza imani na kuwavutia wananchi wengi kujiunga na vifurushi hivyo.

"Tunapokea malalamiko kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma wakidai kuchelewesha madai yao mara wanapotoa huduma, tunaomba mbadilike na kuwa bora zaidi katika kuleta tija kwa jamii," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa mfuko huo, Anne Makinda, alisema wamepokea maoni ya namna bora ya kuboresha mfuko huo.

" Tumepokea ushauri na maeneo yenye matatizo tutayatatua, lakini mwishoni mwa mwezi huu tutaingia mkataba na baadhi ya taasisi za kifedha ili mwanachama anayetaka kujiunga kuwekeza pesa yake kidogo kidogo," alisema Makinda.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, aliitaka NHIF kutazama vifurushi vinavyowahusu wazee kutazamwa upya kwani imeonekana kuwa ni gharama kubwa zaidi.

# Mmea vamizi watishia Moshi, Mwanga

**Na Mary Mosha,** MWANGA

UTAFITI unaonyesha ongezeko la mmea vamizi aina ya mrashia (Prosopis Juliflora) unaopatikana katika wilaya za Mwanga na Moshi umekuwa chanzo cha kupoteza uoto wa asili katika wilaya hizo kutokanana na asili ya mti huo.

Mmea wa mrashia ambao asili yake ni nchini Mexico, umekuwa na madhara makubwa katika sehemu za malisho, hifadhi za wanyamapori na kilimo kutokana na asili yake.

Hayo yalisemwa na Prof. George Kajembe kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) alipokutana na jopo la wataalamu kutoka nchi za Afrika Mashariki wilayani Mwanga ikiwa na lengo la kujenga uelewa kwa wananchi pamoja na kuutumia mti huo kama fursa ili kujiingizia kipato.

Alisema, mmea huo umeathiri pia katika mikoa ya Mwanza, Morogoro, Tanga, Dodoma na Pwani jambo ambalo ikiwa hatua za haraka hazitachukuliwa zinaweza kuleta hadhari kwa jamii hasa katika mabadiliko ya tabianchi.

"Leo tumekutana hapa mkoa wa Kilimanjaro katika Wilaya ya Mwanga, ambapo na jopo la wataalamu wa wataalamu wa mazingira kutoka Afrika Mashariki lengo likiwa kuangalia namna ambavyo tunaweza kuudhibiti mti huo usiendelee kwenye jamii na miti iliyopo kutumika kama fursa kwa jamii husika," alisema. Alisema ikiwa mti huo utatumika vyema unaweza kuwaingizia kipato wananchi kwa kutengeneza lishe, asali na vileo.

Ofisa Mazingira wilayani humo, Neema Mgweno, amekiri kuwapo kwa mmea mrashia maeneo ya tambarare ambapo imeathiri uoto wa asili hususani maeneo yanayozunguka Bwawa la Nyumba ya Mungu.

"Kabla ya tafiti hizi hatukufahamu chanzo cha ongezeko la upotevu wa uoto wa asili katika maeneo ya tambarare, lakini ujio wa tafiti hizi kunaweza kusaidia wananchi kupunguza matumizi ya miti hii kuzaliana," alisema.

Akifungua kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya hiyo, Thomas Apson, amewataka wakazi wa Mwanga kutumia elimu wanayoipata katika kukabiliana na madhara ya mmea huo.

Tubia Bakari, mkazi wa Kijiji cha Langa'ata Bora wilayani Mwanga ambacho kimeathiriwa na mmea wa mrashia alisema elimu waliyoipata juu ya faida za mmea huo utawasaidia kujiongezea kipato ikiwa ni pamoja na kuchukua tahadhari kwa ongezeko la mmea huo ili kutunza mazingira.



Ukurasa 18

Utafiti tofauti unavyoipaisha nchi



Ukurasa 15

Huu hapa ujasiriamali na ubunifu wake ulivyo

# BUFE

Ijumaa Januari 17, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

## Marekani, China walipotia saini kuweka sawa mauzo biashara zao



# Meneja wa Bandari 24 za Viktoria na simulizi ya kukokotoa bilioni 2/-

**Na Elizabeth Zaya,** aliyekuwa

MWANZA

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) katika bandari zake za Ziwa Viktoria, imejipanga kuzitumia kuleta mapinduzi ya kiuchumi.

Miongoni mwa mipango iliyojiwekea katika kufikia malengo hayo, ni kwenda sambamba na uboreshaji unaofanyika katika bandari zote zilizopo Ziwa Victoria.

Meneja wa Bandari hizo, Morris Mchindiuza, anasema tayari wameshatumia Sh. bilioni 16.5 katika miradi yake ya kimkakati kuboresha miundombinu ya Bandari za Ziwa Viktoria, ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Anasema kiasi hicho cha fedha, kimetumika katika kipindi cha miaka miwili lengo, dira kuu ni kuziongezea uwezo bandari hizo ambazo ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi, ndani ya safari kuelekea uchumi wa kati kitaifa.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Pata vigezo vya utata biashara kuporomoka

Ukurasa 20

BIASHARA

MAFAHARI WAYAMALIZA...

# Marekani, China walipotia s kuweka sawa mauzo biasha

Na Mwandishi Wetu

MATAIFA ya Marekani na China yametia saini makubaliano yanayolenga kumaliza vita vya kibiashara, ambavyo vinaelezwa kuathiri masoko na uchumi wa dunia.

China na Marekani zimekuwa katika vita ya kibiashara tangu Rais Donald Trump aingie madarakani na kuanzisha sera ya 'Marekani Kwanza' inayolenga kulinda bidhaa za nchi hiyo.

Rais Trump akizungumzia makubaliano mjini Washington, anasema makubaliano hayo ni mapinduzi makubwa kwa uchumi wa nchi yake ya Marekani, huku viongozi wa China wametaja makubaliano hiyo kama ushindi kwa pande zote na utasaidia kuimarisha uhusiano wa pande mbili.

China imeahidi kuongeza bidhaa zinazouzwa Marekani zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 200 ikiwa ni ongezeko la kiwango ilichoweka mwaka 2017, kisha kuimarisha sheria za haki miliki.

Aidha, Marekani imekubali kupunguza kwa asilimia 50 ya kodi mpya dhidi ya bidhaa za China zinazoingizwa Marekani.



Donald Trump na Makamu wa Rais wa China, Wang Qishan, wakiwa na hati ya makubaliano.



### YALIVYO MAKUBALIANO

Katika mazungumzo hayo, mafahari hao wa uchumi wa dunia, wamekubaliana kuimarisha ununuzi wa bidhaa za kilimo kwa thamani ya Dola za Marekani bilioni 32, uzalishaji kwa Dola bilioni 78, nishati Dola bilioni 52 na huduma nyinginezo bilioni 38.

Pia, China imekubali kuchukua hatua zaidi dhidi ya bidhaa ghushi na kufanya iwe rahisi kwa kampuni kuchukua hatua za kisheria dhidi ya uchukuaji taarifa muhimu za kibiashara.

Marekani imekubali kuacha asilimia 25 ya kodi kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka China zenye thamani ya bilioni 360, ikiwa imeweka kodi mpya kwa bidhaa za Marekani zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 100 na inatarajiwa kuendelezwa kiwango hicho cha kodi.

### YANAAKISI DUNIA?

Makamu Rais wa China Liu He, alitia saini makubaliano kwa niaba ya China, anasema makubaliano hayo yalibebwa na kuwapo usawa na kuheshimiana kwa pande zote mbili hizo za dunia.

Pia katika hutoba yake alitamka kuleta mfumo wa kiuchumi wa nchi yake, kwamba hautakuwa na madhara katika uchumi wa dunia wa sasa.

"China ina mfumo wa kisiasa na wa kiuchumi ambao unaendana na maslahi ya taifa," anasema.

"Hii haimaanishi kwamba China na Marekani haziwezi kushirikiana. Badala yake, nchi hizi mbili zinashirikishana maslahi mengi ya kibiashara," anasisitiza.

> **"Marekani imekuwa chanzo kikubwa cha uwekezaji wa moja kwa moja barani Afrika, lakini mchango wake umekuwa ukipungua.**



Marais, Donald Trump wa Marekani na Xi Jinping wa China, wakipeana mikono ya kirafiki.
**PICHA ZOTE: MTANDAO**

Makamu huyo wa Rais, anaongeza:"Ni matumaini yetu kwamba pande zote mbili zitashirikiana na kutimiza waliokubaliana na kudumisha makubaliano kwa dhati."

Ni aina ya makubaliano yaliyopigiwa makofi kimataifa, kwamba

# aini
# ra zao





mwanzo wa kumalizika vita baridi vya kibiashara duniani.

Rais Trump anasema, ni mazingira yanayotokea katika hali ya kulinda kazi za kampuni za Wamarekani, kutokana na kile anachokitathmini kama "ushindani usiyo wa haki wa kibiashara."

Hali hiyo isiyo ya kawaida, Rais kutia saini mkataba wa pande mbili kunachagiza umuhimu wa mkataba huo kuonekana ushindi kwa Marekani, huku kiwango cha kodi kikifanyiwa marekebisho na maridhiano madogo ya kibiashara yakifikiwa.

Aidha, malalamiko ya Marekani kuhusu kinachoitwa "tabia ya China kuanzisha mtazamo wake, utoaji ruzuku za kibiashara hadi wizi wa kimtandao" bado haijashuhidiwa katika mwafaka huo.

Pia kumekuwapo dai la Rais Trump, ambaye nchini mwake nazi 'hazijapoa' kwake, kutaka kuandikwa tena sheria za kibiashara duniani hazijafanikiwa.

### AFRIKA KULIKONI?

Marekani imekuwa ikipoteza ushawishi barani Afrika, lakini kuna dalili nchi hiyo inataka kubadili hali hiyo, iendelee kulikamata bara hilo.

Mjumbe wa Masuala ya Afrika wa Marekani, Tibor Nagy anatamka: "Ikamate kwa muda mrefu, wakati wawekezaji walipokuwa wakibisha milango na Waafrika wakimfungulia mtu pekee aliyekuwapo, Mchina.

Marekani imekuwa chanzo kikubwa cha uwekezaji wa moja kwa moja barani Afrika, lakini mchango wake umekuwa ukipungua.

> **"Kampuni za China, zimechangia maendeleo makubwa katika ujenzi wa miundombinu mipya na iliyosahaulika kwa muda mrefu katika baadhi ya mataifa ya Afrika.**

Inaelezwa, ushindani kutoka nchi nyingine umeongezeka katika kipindi cha muongo mmoja uliopita bna katika utawala wake, Rais Trump anaelezwa kuinyima amani Afrika kisiasa kwamba 'sehemu ambayo marafiki zake wanakwenda kujaribu kutajirika.'

China nayo mwaka 2018, ilitangaza uwekezaji wa thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 60 kwa ajili ya miradi ya miundombinu Afrika.

Lina Benabdallah, mtaalamu wa uhusiano ya China na Afrika katika Chuo cha Wake Forest, Marekani, anasema biashara kati ya Marekani na mataifa ya Afrika imeshuka kwa sababu ya ongezeko la uhitaji wa China, Russia na Uturuki.

Kampuni za China, zimechangia maendeleo makubwa katika ujenzi wa miundombinu mipya na iliyosahaulika kwa muda mrefu katika baadhi ya mataifa ya Afrika.

Mtaalamu huyo anasema, Marekani imekuwa ikiishtumu China kwamba inahimiza mataifa ya Afrika kujitegemea na ilitumia mikataba ya kifisadi na kuhatarisha rasilmali asili za mataifa hayo.

Pia, anadai imewahi kuutaja uwekezaji wa China kwa Afrika kama wenye uwezo wa kuimarisha miundombinu Afrika, lakini unaongeza madeni na nafasi kidogo za ajira.

Kwa ujumla kibiashaara, inaelezwa Marekani ina wakati mgumu kujihusisha na uchumi wa nchi hizo unaochipukia na wakati huohuo kukabiliana na kasi ya ukuaji uchumi wa China.

***Kwa msaada wa taarifa za kimataifa***

## Huu hapa ujasiriamali na ubunifu wake ulivyo



Wajasiriamali wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

NI vigumu kujadili ujasiriamali, pasipo kuelewa maana yake halisi. Wataalamu wanautafsiri kwamba ni mchakato au utaratibu wa kubuni au kuandaa, kuanzisha na kisha kuendesha biashara mpya. Hivyo, mbunifu huyo ndiye anayeitwa mjasiriamali.

Pia, wanazuoni wanautaja kuwa ni uwezo wa uthubutu wa kuendeleza, kupanga na kusimamia biashara pamoja na changamoto zake za hasara, katika safari ya kusaka faida.

Na ili kufanikiwa, wataalamu hao wanasema kuna kanuni kadhaa za kuzingatia. Kwanza, anatakiwa awe mbunifu ambayo ni kanuni muhimu kwa kila mjasiriamali. Ubunifu hauishii kutengeneza, bali maboresho ya vitu unavyotengeneza.

Ubunifu huo, una sura kuu tatu; ubunifu katika kuendeleza na kuboresha bidhaa au huduma iliyoko sokoni, ubunifu katika kuzalisha kipya, kwa kuzingatia hitaji la soko na ubunifu katika uendeshaji biashara tajwa.

Kanuni ya pili ni nidhamu; mjasiriamali lazima athamini kazi yake, muda na pesa inayopatikana, akifanya hilo kwa kujinyima na kujibana, kufikia malengo makubwa kikazi.

Tatu, ni budi awe sehemu ya shughuli zake na mahitaji ya bidhaa au huduma hiyo katika eneo hilo kwa kwa wateja wake, katika eneo unakofanya shughuli zake.

Mfano huwezi kuuza bidhaa, ambayo katika mahali husika ni marufuku. Ni lazima eneo hilo liwe na uhitaji wa huduma au bidhaa inayotakiwa.

Nne, bidhaa au huduma husika inapaswa iendane na thamani ya bidhaa au huduma, maana bei ya bidhaa au huduma inaweza kumvuta mteja au kumfukuza. Ni lazima bei ilingane na thamani ya bidhaa au huduma au bidhaa, pia nguvu za kiuchumi za wateja.

Tano, matangazo ya bidhaa au huduma kwa mjasiriamali, lazima yahakikishe yanatengeneza mtandao wa wateja kujua bidhaa au huduma iliyoko sokoni, kwa njia mbalimbali zinazofaa.

Haitoshi kama mjasiriamali kutengeneza bidhaa nzuri au kuwa na huduma nzuri, lakini jirani zako hawajui na hawana taarifa ya bidhaa yako au huduma yako ndio maana unaona matangazo ya biashara kwenye vyombo vya habari Tv na redio kila mara.

Ndio maana unaona nchi yetu inajitahidi kutangaza vivutio vya utalii huko kwenye nchi zingine ili waujue Mlima Kilimanjaro upo Tanzania, mbuga za wanyama wa kila aina na kadhalika wanasema 'biashara ni matangazo.'

Mjasiriamali lazima utangaze bidhaa yako au huduma yako kwa njia yoyote ili iwafikie wateja wengi kadri iwezekanavyo.

Maneno ya hamasa na kutiana moyo na historia za watu waliofanikiwa za kutokata tamaa, kujituma, kujiamini, sijui nini haya yote yakuwa na umuhimu na faida pale utakapokuwa umetimiza kanuni za ujasiriamali na biashara yako ili usipoteze fedha zako na mikopo ukauziwa dhamana zako bure.

**Kwa mujibu mtandao**

BIASHARA

# Meneja wa Bandari 24 za Viktoria na simulizi ya kukokotoa bilioni 2/-

## • Adai ameapa na lazima kutimiza • Sh. bilioni 8 zimeshaingia mfukoni • Vyanzo kuu sita, vidogo 18; mikoa minne



Bandari ndogo ambazo TPA inazisimamia kwa karibu.

INATOKA UK.13

Mchindiuza anasema mikoa inayozungukwa na mikoa, ina bandari kuu sita na ndogo 18, zinazojumuisha bandari kuu za ziwa, ikiwamo ni pamoja na Mwanza Kaskazini, Mwanza Kusini, Nansio, Kemondo Bay, Bukoba na Musoma.

Mchindiuza anasema, kwa sasa miradi mingi inaendelea kutekelezwa na ipo iliyokamilika kwa asilimia 100 na mingine iko katika hatua za mwisho.

**MAKUBWA?**

Meneja Mchindiuza anataja anayoyaita 'mambo makubwa' yaliyofanyika katika maboresho hayo, ni pamoja na ujenzi wa magati, maghala, madaraja ya kuunganisha reli na meli, nyumba za kupumzikia abiria, vyoo, vyumba vya walinzi na ununuzi wa mitambo ya kuhudumia shehena.

Pia mengine anajumuisha uboreshaji mradi mkubwa wa bandari kavu ya Fela, uliopo katika hatua ya utwaaji wa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 1,178 kutoka kwa wananchi ambao tayari hatua hiyo imekamilika, wakazi jirani kulipwa fidia kiasi cha Sh. bilioni 5.6.

Miradi mingine anaitaja ni ujenzi wa magati na thamani yake katika mabano; Lushamba (Sh. bilioni 1.2), Ntama (Sh. bilioni 2.2), Mwigobero (Sh. milioni 605) na Nyamirembe (Sh. bilioni 4.1).

Mchindiuza anataja ukarabati mwingine anautaja ni ujenzi wa jengo la ofisi na abiria awamu ya pili Sh. milioni 143.8, ujenzi wa gati la Magarini Sh. bilioni 1.7 na ukarabati wa daraja la Link Span katika Bandari ya Kemondo Bay Sh. milioni 815.7.

> **"Hapa vinaangaliwa vitu vingi, eneo linapokuwa bandari hiyo bubu, mazingira kama ni salama au si salama, na zile ambazo zitakuwa na sifa zitarasimishwa na kuingizwa kwenye mfumo maalum wa usimamizi.**



Sehemu ya Bandari ya Musoma. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**MATOKEO CHANYA**

Meneja huyo anasema maboresho yameanza kuleta matokeo chanya, kwani katika kipindi cha miaka miwili, tayari shehena pamoja na mapato vimeongezeka maradufu.

"Katika kipindi cha miaka mitano 2014/15 hadi 2018/19 shehena iliyohudumiwa katika Bandari za Mwanza imekuwa ikipanda kwa wastani wa asilimia 0.5 kutoka tani 129,767 mwaka 2014/15 hadi tani 157,808 mwaka 2018/19," anasema Mchindiuza na kuongeza:

"Katika kipindi cha miezi minne ya kwanza ya mwaka 2019/20 Julai hadi Novemba mwaka jana tumehudumia tani 76,168 ikiwa ni sawa na asilimia 99.14 ya lengo la kuhudumia tani 76,833."

Pia anataja sababu zingine za kupanda shehena zinazosafirishwa ni kuendelea kuimarika reli ya kati, zikiwamo shehena za mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda Uganda, sambamba na kufunguka biashara katika ushoroba wa wanyama Ukanda wa Kati.

Mchindiuza anasema, jitihada za masoko zilizofanyika kurejesha wateja wakubwa waliokuwa wanatumia barabara ina nafasi katika mageuzi hayo ya kimasoko, sasa wakiumia huduma za meli, hatua iliyoiongezea TPA mapato kutoka Sh. bilioni 1.133 katika mwaka wa fedha 2014/15 hadi Sh. bilioni 1.422 mwaka 2018/19.

**MATARAJIO**

Mchindiuza anasema, matarajio yajayo ni kwamba katika mwaka uliopo wa fedha uliopo mkakati waliojiwekea ni kuingiza mapato ya Sh. bilioni mbili na katika robo ya kwanza ya mwaka huo, ambayo ni kati ya Julai hadi Novemba mwaka jana walikusanya Sh. milioni 802.

Anasema matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) katika makusanyo, yamesaidia kuongeza mapato katika bandari wanazotumia mfumo huo, ambazo ni: Kemondo Bay na Mwaloni, Kyamkwikwi, Mwanza Kaskazini na Kusini, Isaka, Mwigobero Bukoba na Mwalo wake na Nansio.

Mikakati mingine anaitaja ni kuhakikisha wanafikia lengo kubwa la bandari, kuwa lango kuu la uchumi wa nchi katika ukanda huo wa Ziwa Victoria ni kukomesha utitiri wa bandari bubu katika eneo hilo.

Anasema, tathmini waliyoifanya hivi karibuni, bandari bubu katika ziwa hilo zinafikia 300 katika kuhakikisha bandari hizo za Kanda ya Ziwa na zinaongeza ukusanyaji mapato, kutokana na huduma inazotoa, wameamua kuzitambua.

Meneja anasema katika kuzihakiki na kuzitambua bandari hizo, zipo baadhi ambazo zitafutwa kabisa na nyingine ambazo zitakidhi vigezo zitaingizwa katika mfumo maalum wa usimamizi.

"Hapa vinaangaliwa vitu vingi, eneo linapokuwa bandari hiyo bubu, mazingira kama ni salama au si salama, na zile ambazo zitakuwa na sifa zitarasimishwa na kuingizwa kwenye mfumo maalum wa usimamizi," anasema Mchindiuza.

Anaongeza: "Tumebaini kwamba bandari hizi ndizo zimekuwa zikitumika kupitisha bidhaa haramu na kwa sababu tumepakana na nchi nyingi jirani katika ziwa hili, hatuwezi kuruhusu hali hii iendelee. Tunazirasimisha na zitasimamiwa na mamlaka zote ikiwamo zinazohusika na afya na nyinginezo zitakuwapo katika kila bandari."

Mchindiuza anasema, mbali na kudhibiti bandari bubu, pia TPA imepewa jukumu ya kuendeleza bandari, kuendesha, kutangaza huduma zake kwa kushirikiana na sekta binafsi katika uendeshaji wake.

Anasema meneja wa bandari zilizopo ukanda huo, amejiwekea malengo kuleta mageuzi ya kiuchumi, kupitia bandari katika ukanda wa ziwa hilo.

"Unajua kipindi cha nyuma bandari nyingi zilikufa, lakini serikali ya awamu ya tano imeamua kuzifufua, na kwa jambo hilo sisi watendaji wa TPA tumeamua kupambana, kuendeleza juhudi hizi alizozianzisha Rais wetu Dk. John Magufuli.

"Kwa Ziwa Viktoria nimejiwekea malengo ya kuhakikisha bandari zetu zinaboreshwa na kuwa za kisasa kwa lengo kubwa moja la kuleta mapinduzi ya kibiashara," anasema Mchindiuza.

"Hili ni lengo ambalo nimeapa na lazima litimie, lazima tuhakikishe bandari zote zinafufuka na kufanya kazi saa 24, miundombinu hii tunayoiboresha, naamini hakuna mfanyabiashara atayeshindwa kufanya kazi na sisi na tumewaandalia mazingira mazuri ya kibiashara katika bandari zote za ziwa hili," anasema.

Mchindiuza anasema, TPA inaweka mkakati kukusanya mapato ya ndani kwa kuhakikisha wafanyabiashara wa uhakika ambao wanatumia bandari, kwa sababu usafirishaji wa majini una gharama nafuu zaidi.



Daraja la reli linalotumika kupitisha mizigo inayopakiwa katika behewa, kisha kuingizwa melini katika Bandari ya Kemondo Bay, Mkoa wa Kagera.

# Biashara katika picha



Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mkuu wa Kanda ya Mashariki wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Lawi Odiero (mwenye miwani), akimkabidhi moja ya kompyuta 10 na vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) Mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro ambaye ni Ofisa Taaluma wa Mkoa huo, Tullo Fundi, katika hafla iliyofanyika Shule ya Sekondari Mzumbe. Katikati anayeshuhudia mwenye suti ni Makamu Mkuu wa shule hiyo, Edwin Matenga. **NA MPIGAPICHA WETU**



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya I&M, Baseer Mohammed, akizungumza baada ya kukabidhi msaada wa meza na viti 100 kwa Shule ya Sekondari Mrisho Gambo iliyopo mkoani Arusha, jana, kupitia sera yake ya kurudisha faida kwa jamii. Wengine ni Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Joyce Ndalichako, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (wa pili kushoto) na Meneja wa Wateja Binafsi, Lilian Mtali. **NA MPIGAPICHA WETU**



Meneja wa Kitengo cha Kadi CRDB, Antony Siyovelwa, akifanya manunuzi kwa njia ya Tembo Card Visa katika duka la GSM Mlimani City jijini Dar es Salaam, leo, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Tembo Card Visa ijulikanayo kama "Chanja, Lipa, Sepa". **NA MPIGAPICHA WETU**

UCHUMI

# UTALII TOFAUTI UNAVYOIPA

- Hifadhi mpya za kitaifa mtaji • Kituo cha Singida chaja na upekee
- Wizara Utalii yatoa takwimu za kupaa • Dk. Kigwangalla: Ndege inatubel
- RC Dk. Nchimbi: Singida mambo safi




Watalii wakishuhudia vivutio mbugani. **PICHA: MAKTABA**

**Na John Mapepele**

RAIS John Magufuli, amekuwa akiitambulisha Tanzania nchi yenye utajiri mwingi inayostahili kutoa misaada kwa mataifa mengine, badala ya kuwa ombaomba.

Amekaririwa na vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi, akisisitiza Tanzania ina aina nyingi za madini yakiwamo tanzanite inayopatikana nchini pekee, eneo kubwa lenye rutuba linalofaa mazao; mito maziwa na ukanda wa bahari na vivutio utalii, baadhi haviko kwingine visivyopatikana sehemu yoyote duniani. Tanzania ni ya pili duniani kwa kuwa na vivutio vya utalii.

Inao utajiri wa hali ya hewa ya kuvutia; rasilimali kutosha, mifugo mingi ikishika nafasi ya pili kwa Afrika, ni nchi yenye amani na usalama na kijiografia ipo kimkakati kama lango la kuingia nchi sita ambazo hazina bahari. Uwepo wa raslimali zote hizi zinatoa fursa nyingi za uwekezaji.

Aidha, mapambano ya rushwa na ufisadi; ukuaji uchumi endelevu, ujenzi wa viuwanda; kurekebisha sheria na mikataba ili nchi inufaike na raslimali zake; ujenzi wa mazingira mazuri ya biashara, utekelezaji wa diplomasia ya uchumi na utekelezaji wa miradi mikubwa kwa kutumia fedha za ndani vimeipa nchi heshima kubwa na kujenga taswira nzuri kimataifa.

> **Idadi ya watalii wanaoingia nchini imeongezeka hadi kufikia milioni 1.5 mwaka 2018 kutoka milioni 1.3 mwaka 2017.**

Uanzishwaji wa mbuga na hifadhi za wanyama na mara kadhaa kunapokewa ndege zinazonunuliwa na serikali, Rais Magufuli akisema serikali imejipanga vyema kuhakikisha nchi yetu inakuwa na ndege za uhakika, zitakazosaidia kuwaleta wageni moja kwa moja nchini, kutembelea vivutio vya kitalii.


**WAZIRI KIGWANGALA**

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangala, anasema usafiri wa anga unachochea ukuaji utalii nchini, akirejea mwaka 2018, takribani asilimia 62 ya watalii waliotembelea nchini walitumia usafiri huo na asilimia 37 walitumia barabara. Reli na maji ilbeba



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, katika uzinduzi wa Kituo Utalii wa Hija. **PICHA: JOHN MAPEPELE.**

# AISHA NCHI



o cha



Siku Rais John Magufuli alipoongoza viongozi kupokea ndege ya Shirika la Ndege Tanzania, katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

chini asilimia moja.

Anasema, katika kipindi hicho Rais Magufuli, amekuwa akiwateua mabalozi na kuwasisitiza kazi iliyoko mbele yao, ni kuiwakilisha vyema nchi na kutangaza fursa na vivutio kitaifa, ili kuliingizia taifa mapato. Ni utekelezaji wa diplomasia ya uchumi.

**SIFA YA NCHI**

Kumeshuhudia udhibiti mkubwa wa mapato ya serikali na kupunguza safari zisizo na tija za viongozi nje ya nchi, Rais mwenyewe akiwa mfano.

Wakati wa Mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika hivi karibuni nchini, Rais Magufuli, alikabidhiwa uenyekiti wa SADC, wakuu wote wa nchi wanachama wa SADC, walipongeza juhudi zinazofanywa na serikali kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi.

Katika hotuba yake ya kwanza baada ya kusimikwa uenyekiti, Rais Magufuli aliwakaribisha wageni kutoka katika nchi wanachama kutembelea na kuona vivutio mbalimbali ya utalii hapa nchini.

Ni ukweli usiopingika Tanzania sasa ni eneo linaloaminika zaidi kuwekeza kutokana na mazingira yaliyowekwa katika sekta nyingi, takwimu zinaonyesha kuwa hata idadi ya watalii imekuwa ikipanda ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Profesa Adolf Mkenda, anasema idadi ya watalii wanaoingia nchini imeongezeka hadi kufikia milioni 1.5 mwaka 2018 kutoka milioni 1.3 mwaka 2017.

Hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 13.5 na alisema ongezeko hilo ni kubwa sana.

**KIVUTIO KIPYA**

Wakati tunaanza mwaka 2020, Tanzania imeingia katika historia mpya kuzindua kivutio kingine kikubwa cha utalii wa kiroho katika Mkoa wa Singida.

> **“Uzinduzi wa kituo cha Hija cha Bikira Maria siyo tu kwamba utabadilisha kabisa uchumi wa watu wetu bali utasaidia nchi yetu kukuza amani ambayo ni mhimili mkuu wa maendeleo ya taifa lolote duniani.**



Hafla ya kuzinduliwa Kituo cha Utalii wa Hija. **PICHA: JOHN MAPEPELE.**

Ni kivutio kituo cha kikubwa cha Hija kilichozinduliwa Januari Mosi mwaka huu katika eneo la Sukamahela kutokana na ubunifu wazo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi.

Dk. Rehema Nchimbi amesema uzinduzi wa kituo kikubwa cha kihistoria cha Hija na maombezi kilichojengwa eneo la Sukamahela ambalo ndiyo eneo la katikati ya nchi ya Tanzania kijiografia wilayani Manyoni utabadilisha uchumi na kuchochea maendeleo ya Tanzania.

Dk. Nchimbi anaamini uzinduzi wa kituo hicho, unaifanya nchi kuongeza idadi ya vivutio vya utalii wa imani ambao haukuwapo kabisa nchini, hivyo kuvutia wageni kutoka sehemu mbalimbali duniani wanaokuja kutembelea maeneo mbalimbali ya mbuga na hifadhi za wanyama na bahari kujumuisha eneo hilo.

Anasema, aneo hili ni la kihistoria na kimkakati kwa kuwa ndiyo eneo la katikati ya Tanzania ambalo pia lipo karibu na makuu makuu ya nchi na kama litatangazwa vizuri, ni fursa kubwa hata kwa wageni mbalimbali wanaofika makao makuu kutembelea na kufanya hija.

Dk. Nchimbi, anatoa rai kwa wananchi kufanya uwekezaji katika eneo hilo kwenye sekta za utoaji wa huduma, ili kunufaika na wageni wanaofika kujihi kutoka sehemu mbalimbali duniani na kuunga mkono jitihada za Rais Magufuli, kuwaletea maendeleo.

“Uzinduzi wa kituo cha Hija cha Bikira Maria siyo tu kwamba utabadilisha kabisa uchumi wa watu wetu bali utasaidia nchi yetu kukuza amani ambayo ni mhimili mkuu wa maendeleo ya taifa lolote duniani,” aliongeza.

Mkuu huyo wa mkoa anaongeza: “Tusichoke kumkimbilia, tusichoke kumwomba amani ya taifa letu kupitia sala na maombezi yake.”

**UZINDUZI**

Akizindua kituo hicho Januari Mosi mwaka huu, Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Singida, Mhashamu Edward Mapunda, alishukuru na kupongeza wazo la Mkuu wa Mkoa wa Singida Dk. Nchimbi, imani.

Askofu Mapunda kupitia Mkuu wa Mkoa, alimshukuru Rais John Magufuli kwa mchango wake katika kufanikisha ujenzi wa kituo hicho cha hija, alioutoa hivi karibuni akiwa safarini wakati alipopita mkoani hapa kuelekea chato mkoani Geita kwa mapumziko.

Desemba 9 ya kila mwaka ndiyo imepangwa kuwa siku rasmi kukusanyika kitaifa. Kituo cha kwanza kilichopo eneo la Kimbwi nje kidogo ya mji, ambacho pia kwa lengo lile lile hutoa fursa ya watu kukutana kiimani.

BIASHARA

# Pata vigezo vya utata biashara kuporomoka

## • Utafiti: Nusu miradi inakufa kabla ya miaka kumi



Biashara zilizoshamiri Kariakoo jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

UTAFITI wa usimamizi wa biashara, unaonyesha kuwapo tabia nusu ya biashara zinazoanzishwa, zinakufa kabla ya miaka mitano, theluthi ndio zinafanikiwa kufikisha miaka 10. Kwa kifupi, ni nusu pekee za biashara ndio zinavuka safari hiyo.

Jarida la Forbes kwa msaada wa utafiti uliofanywa na channel za kibiashara inaonyesha biashara nane kati ya 10 (asilimia 80) hufa ndani ya mwaka mmoja na nusu.

Nini chanzo chake? Kuna sababu kadhaa zinazoorodheshwa

### TATIZO USIMAMIZI

Uongozi dhaifu unaweza kudhihirisha kuwa mizozo ya kila mara baina ya viongozi wa timu yao ya kazi, kukinzana maoni ni tatizo.

Inaelezwa hatari ya kufanya uamuzi unaochelewa, au tatizo kutoshughulikiwa kwa wakati sahihi, ndivyo mwanzo wa biashara kulega.

Hatua stahiki hapo, ni kukubali kujifunza, kusoma mbinu za uongozi kadri iwezekanavyo hata kuhudhuria madarasa husika. Tafuta mwalimu binafsi wa biashara (mentor), fanya utafiti binafsi na kila aina ya mbinu kunyanyua uwezo wako wa kuongoza, kisha zichanganue mbinu zote za uongozi na chagua iliyo bora kwa biashara yako.

> **Kuanzisha biashara ni jambo la kusisimua sana na linahitaji bidhaa au huduma iliyojikamilisha, kwa kuwepo huduma au bidhaaa hiyo sokoni.**

### THAMANI PEKEE

Wakati mtu anaweza kuwa na bidhaa au huduma bora inayohitajika sana sokoni, bado anafanya vibaya sokoni. Huenda kunakoseka kuonyeshwa thamani ya bidhaa sokoni au ina washindani wengi, kuifanya bidhaa yako kuwa juu sokoni.

Swali la msingi hapo ni kujiuliza, kitu gani kinakutofautisha na wapinzani wako, unatumia mbinu gani kuwa tofauti na wenzako, washindani wako wanafanya nini hata kuikushinda?

Baada ya kuyajua hayo, boresha biashara na tengeneza mfumo na kifurushi cha huduma ambayo hakuna mwingine anaitoa katika soko, kiasi itachukua umakini wa wateja na kuwafanya waipende huduma au bidhaa yako.

Hivyo ndivyo vitatengeneza chapa yako na ndio inatoa taswira ya huduma yako kwa mteja kuitumia chapa hiyo. Itumie chapa hiyo, kwani ndio utambulisho wako; rangi au, kaulimbiu na vitu vingine vinavyoonekana, ikiwamo sera.

Kimsingi, sera ni lazima iwakilishe thamani ya bidhaa au huduma inayotolewa.

Ili kuifanya chapa yako ifahamike, lazima utumie mbinu nyingi za masoko na usiogope kusimama kwenye matukio ya kijasiriamali kuongea au kuweka vipeperushi vyako.

### MAWASILIANO DUNI

Kupuuza wanachosema wateja au kutokuwa karibu nao, ni dhahiri biashara italega. Inashauriwa kuwa karibu na wateja na kuyaelewa mahitaji na mrejesho wanaokupatia.

Wateja wanaweza kuipenda bidhaa au huduma itolewayo, wangeipenda zaidi kama kitu fulani kingeboreshwa. Cha kufanyika hapo ni aliyefanikiwa, huweka mkazo katika bidhaa iliyoko sokoni kujua wateja muhimu na wanavutiwa vipi na bidhaa au huduma hiyo na utengeneze njia bora ya kusimamia uhusiano na wateja.

### MFUMO USIOFAIDISHA

Moja ya viashiria vikubwa vya kuanguka biashara, ni kuwapo mfumo thabiti wa kuendesha biashara ni mpango kazi na 'kukomaa' na safari ya tija, kwani wazo la biashara linaweza kuwa zuri, lakini kukosekana mikakati ya uongozi kunachangia kuanguka biashara hiyo.

Muhimu hapo ni kutafuta utafiti na rejea, kisha kutengeneza mfumo kamili wa mpango wa biashara ambao unahusisha makadirio ya mapato yanayotegemewa, mikakati ya masoko na ufumbuzi wa changamoto za usimamizi katika kuvivuka vikwazo muhimu vya masoko na wapinzani.

Andaa jedwali linaloonyesha kazi husika na malengo yaliyoambatanishwa na ukomo wa muda. Ili kuweza kuyapima mafanikio, kutatua changamoto zinapojitokeza na kubaki katika njia sahihi. Mpango kazi thabiti unahusisha mbinu sahihi na unasaidia biashara yako kutoanguka.

### KUSIMAMIA FEDHA

Ili kufanikisha biashara, fedha inayopatikana na kutumika isimamiwe. Ni vyema kuandaa fungu la dharura kuokoa majanga ya fedha au biashara yanapojitokeza.

Mara nyingi watu huanzisha biashara wakiwa na ndoto za kutengeneza fedha, lakini hawana ujuzi wa usimamizi wa mzunguko wa fedha, kodi na gharama.

Utatuzi bora ni kuhifadhi kumbukumbu za fedha na miamala yote, ikiwamo kujumuisha matumizi na mapato yote, kisha kutumia taarifa kutengeneza jedwali la faida na hasara, zitakazosaidia kuonyesha mwenendo wa biashara.

### UKUAJI GHAFLA

Kuna wakati biashara mpya inakuwa kuliko inavyoweza kustahimili. Unaingiza bidhaa sokoni na ghafla unapokea maombi mengi kuliko unavyoweza kuhudumia.

Pia mambo yanakuwa tofauti, unashawishika kuwa bidhaa zako zitauza sana na unaweka bidhaa nyingi ghalani, mwishowe soko linakuwa tofauti na mtu anabaki kutapatapa, bila namna ya kujinasua.

Kukua na kupanuka biashara kunahitaji umakini wa mipango na mikakati unaohusisha usimamizi wa uzalishaji wa siku baada ya siku, ikihusisha utafiti katika kupima mgawanyo wa watu katika eneo husika na kiwango cha mapato.


Aina ya bidhaa na mipango endelevu ya eneo husika.

Tafiti hizi pia lazima zijiridhishe kuwa wakati ni sahihi na fedha kwa mpango huo zipo.

Mmiliki anatakiwa ahakikishe biashara iliyopo ni imara kabla ya kuanza kujitanua, pia asiongeze bidhaa ambazo hana uhakika kuziuza. Kuanzisha biashara ni jambo la kusisimua sana na linahitaji bidhaa au huduma iliyojikamilisha, kwa kuwepo huduma au bidhaaa hiyo sokoni.

Kama una mpango wa kuanzisha biashara au tayari una biashara yafaa ujue kuwa mafanikio yako yanategemea umakini wa mipango na mikakati yako na umakini wa usimamizi wa fedha tangu mwanzo mpka mwisho wa biashara.

*** Ni kwa mujibu wa taarifa za biashara mtadaoni***





Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Saad Mtambule (katikati), akizungumza wakati wa uzinduzi wa vitabu vitatu vya miongozo ya maendeleo ya Jiji hilo, juzi. Kushoto kwake ni Mkurugenzi Mkazi wa USAID nchini, Andrew Karas na Naibu Meya, Fanuel Kyanula. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Jiji lazindua vitabu vya mwongozo wa maendeleo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imezindua vitabu vitatu vya miongozo ya maendeleo ambavyo vitatumika kama dira ya utekelezaji wa mipango mbalimbali ikiwamo ukusanyaji wa mapato na uwekezaji.

Vitabu hivyo vimeandaliwa na wataalamu wa jiji hilo kwa kushirikiana na Mradi wa Kuwezesha Ukuaji kupitia Biashara na Uwekezaji (Engene) chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Watu wa Marekani (Usaid).

Akizungumza juzi wakati wa uzinduzi wa vitabu hivyo uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Mkapa, Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Saad Mtambule, alivitaja vitabu hivyo kuwa ni vya Mkakati wa Kukuza uwekezaji, Mpango wa Kuongeza Ukusanyaji wa Mapato, na Mpango Mkakati.

Mtambule alisema baadhi ya vitabu hivyo vimeshaanza kutumika kwenye shughuli za maendeleo ikiwamo ukusanyaji wa mapato na kwamba matokeo yake yameanza kuonekana kwa mapato kuongezeka.

Alisema kitabu cha Mpango Mkakati wa Jiji la Mbeya kitatumika kwa muda wa miaka mitano na kilianza kutumika mwaka jana na ukomo wake ni mwaka 2024.

"Mpango mkakati wa mwisho wa jiji letu uliisha mwaka 2008 na mpango wa ukusanyaji wa mapato uliisha 2012. Baadhi ya mambo tulikuwa tunafanya kwa uzoefu tu. Tunashukuru hawa wenzetu wa Mradi wa Engene kwa kutusaidia kuandaa vitabu hivi ambavyo vitatusaidia," alisema Mtambule. Alisema vitabu hivyo vitawasaidia kwa sababu kuna baadhi ya wataalamu wa jiji hilo wameshafundishwa na watakuwa na uwezo wa kuandaa wenyewe vipya baada ya hivyo kufikia mwisho na kwamba hata kwenye uandaaji kulikuwa na ushirikishwaji mzuri.

Mkurugenzi wa Mradi wa Engene, Rod Karvajal, alisema mbali na kuisaidia Halmashauri ya Jiji hilo kuandaa vitabu hivyo, pia wamekuwa wakishirikiana nayo kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Alisema tangu mwaka 2017 mpaka sasa, wamefanya midahalo 19 ya kujadili mambo mbalimbali yanayoathiri biashara na uwekezaji ndani ya Jiji la Mbeya ikiwamo masuala ya sera na utawala.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kutokana na midahalo hiyo baadhi ya mambo yameanza kubadilika ikiwamo ongezeko la ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwenye shughuli za maendeleo na ushirikiano ambao alidai awali ulikuwa wa kiwango cha chini.

"Baadhi ya mambo ambayo yalikuwa yanajadiliwa kwenye midahalo yetu ni kodi ya huduma, leseni za biashara na usajili, mikakati ya kukuza uwekezaji na uboreshaji wa baadhi ya sheria ndogo za halmashauri ambazo ni kikwazo kwa shughuli hizo," alisema Karvajal. Alisisitiza kuwa baadhi ya mambo hayo pia yameainishwa kwenye vitabu vyote vitatu vilivyoandaliwa kwa ajili ya miongozo ya jiji hilo.

# Wanafunzi 1,400 hawajaripoti sekondari

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

ASILIMIA 56 ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka huu katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, hawajaripoti shuleni kutokana na kile kinachodaiwa kuwa ni mwamko mdogo wa wazazi kwenye elimu.

Hayo yalisemwa juzi na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Cathbert Mwinuka, wakati wa mwendelezo wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kukagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Mwinuka alisema wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza walikuwa 2,476 lakini walioripoti shuleni ni 1,132 ambao ni sawa na asilimia 44.3 na ambao hawajaripoti ni 1,404 ambao ni sawa na asilimia 56.7.

Alisema kutokana na hali hiyo, halmashauri imeanza mikakati ya kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa wanaanza masomo ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wazazi kuwapeleka watoto wao shuleni.

"Lakini tumewaagiza watendaji wa kata kuhakikisha wanawafuatilia wanafunzi hao ili wote waripoti kwenye shule walizopangiwa. Hawa waliochaguliwa miundombinu inawatosheleza isipokuwa wale ambao wanasubiri vyumba vikamilike," alisema Mwinuka.

Alisema wanafunzi ambao majina yao yamezuiwa kwa ajili ya kusubiri vyumba vya madarasa vikamilike ni 261 na watajiunga baada ya kukamilika ujenzi wa vyumba sita.

Kwa mujibu wa Mwinuka, vyumba hivyo viko katika hatua mbalimbali za ujenzi na kwamba mpaka Januari 30, vitakuwa vimekamilika na kuanza kutumika.

Baada ya taarifa hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, aliwataka wazazi wote wenye watoto waliofaulu kuwajibika kwa kuwapeleka watoto hao shuleni kabla serikali haijaanza msako wa nyumba kwa nyumba.

Alisema katika wilaya hiyo kuna tabia ya baadhi ya wazazi kukwepa kuwasomesha watoto wao shule na badala yake wanawaozesha huku baadhi wakiwatumikisha watoto wao wa kiume kwenye kilimo, kuchunga mifugo na kufanya shughuli za migodini.

"Kwa mujibu wa sheria, mtoto yeyote anastahili kusoma shule na kwamba kwa takwimu zilizotolewa za watoto ambao hawajaripoti shuleni ni lazima hatua za kisheria zianze kuchukuliwa haraka," alisema.

Mahundi aliwataka wazazi wote kushirikiana na serikali kuwafuatilia watoto hao kwa maelezo kuwa bila ushirikiano wao serikali haiwezi kufanikiwa kwa asilimia 100.

# Latra yasitisha huduma usafiri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (Latra) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imesitisha huduma ya usafirishaji kwa kampuni nane za mabasi ya mikoani baada ya kubaini kuchakachua na kuharibu mifumo ya kuratibu mwendo wa mabasi (VTC).

Aidha, mamlaka hiyo imewataka wamiliki wa kampuni hizo kuvifanyia matengenezo vifaa hivyo ndani ya mwezi mmoja sambasamba na kutekeleza maagizo ziliyopewa na kwamba endapo zitashindwa, zitawajibishwa kwa mujibu wa sheria za usafirishaji.

Meneja wa Latra Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Denis Daudi, aliiambia Nipashe jana kuwa walifanya uchunguzi na ufuatiliaji wa mienendo ya mabasi hayo barabarani kwa kutumia mifumo ya VTC tangu Desemba, mwaka jana, na kubaini ving'amuzi vilivyofungwa havifanyi kazi.

Alisema baada ya ving'amuzi hivyo kuchakachuliwa madereva wa magari hayo walikuwa wanaendesha kwa mwendo mkali, hivyo kuhatarisha maisha ya abiria wao pamoja na watumiaji wengine wa barabara.

"Tulianza kabla ya sikukuu za mwisho wa mwaka jana ili kujiridhisha na huduma ya usafiri wanayopata wananchi kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine. Tuligundua wameharibu mifumo hiyo kwa makusudi kwa lengo la ushindani wa kukimbiza mabasi barabarani jambo ambalo linahatarisha usalama kwa hiyo tumeyasitishia huduma," alisema.

Daudi alisema miongoni mwa hatua ambazo zitachukuliwa endapo wamiliki hawatatekeleza maelekezo waliyowapatiwa ni pamoja na kulipa faini ya Sh. 200,000 mpaka Sh. 500,000, kufutiwa leseni za usafirishaji na kufikishwa mahakamani.

Alisema vifaa hivyo vilivyofungwa kwenye mabasi ni mali ya serikali na kitendo cha madereva kufanya uharibifu ni kinyume cha sheria, hivyo akatoa onyo kwa wamiliki wa mabasi kucheza na mifumo yake.



HABARI DODOMA

# Viongozi masoko sasa watwishwa zigo la usafi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka viongozi wa masoko kuzingatia usafi wa mazingira ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Aidha, amewataka kufuata kanuni na sheria ili kutatua kero zinazowakabili.

Yuna alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na viongozi wa soko la Bonanza, alipofanya ziara ya kukagua masoko na kuhimiza suala la usafi wa mazingira. Alisema suala la usafi kwenye masoko ni muhimu hususan wakati wa msimu wa mvua ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu yanayotokana na uchafu.

Pia alisema ili viongozi hao wanatakiwa kufuata kanuni na sheria, huku wakishirikiana na halmashauri ili kutatua kero zinazowakabili.


Alisema ili kufikia malengo, wanatakiwa kuwatumikia wafanyabiashara wenzao kwa umoja, badala ya kuwagawa kwenye matabaka ambayo yanasababisha migogoro isiyo rasmi.

"Ninawasihi viongozi ndani ya masoko ya jiji kuwa na maono na mtazamo wa mbali kwenye biashara mnazofanya badala ya kujiingiza kwene migogoro na kushindwa kufikia malengo yao na kwa wafanyabiashara wanaowaongoza," alisema.

Naye Mwenyekiti wa soko la Bonanza, Mwita Mabucha, alisema kuwa kwenye soko hilo bado linakabiliwa na kero kubwa ya miundombinu kutokana na maji kutuama na kusambaa kwenye maeneo ya kufanyia biashara.

Mabucha aliomba uongozi wa halmashauri kutatua suala hilo ili wafanye biashara zao kwenye mazingira rafiki.

"Katika soko hili la Bonanza kuna baadhi ya maeneo siyo rafiki kwa wafanyabiashara na wateja wanaofika kupata huduma, maeneo hayo yamekuwa yakituama maji na kusababisha kuleta adha hasa katika kipindi hiki cha mvua zinazonyesha," alisema.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto), Dk. John Jingu, akitoa maelezo kuhusu Sera ya Wazee ya Mwaka 2003 ambayo inafanyiwa mapitio ili kuiboresha wakati alipofungua kikao cha wadau wanaoshughulikia huduma na haki za wazee, jijini Dodoma jana. **PICHA: WIZARA YA AFYA**

# Wabunge wakunwa ujenzi wa ofisi NEC

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeridhishwa na ukamilishwaji wa mradi wa ujenzi wa ofisi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) jijini Dodoma kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Aeshi Hilaly, baada ya kamati hiyo kukagua hatua ya mradi huo katika eneo la Njedengwa jijini hapa.

Alisema kamati imeridhishwa na hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa jengo kuu la ofisi, jengo la kutangazia matokeo na ghala la kuhifadhi vifaa.

"Tunaipongeza serikali kwa hatua ilizozichukua kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu katika kuhakikisha kuwa ujenzi wa ofisi hizi unakamilika kwa wakati, kimsingi ni nia njema kamati kutembelea miradi ya serikali, lakini tunapoona inafanya vizuri hatuna budi kuipongeza na ni imani yetu kuwa kwa malengo iliyoyaweka mwezi Aprili mwaka huu hatua kubwa ya utekelezaji itakuwa imefikiwa," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Anthony Mavunde, alisema wanatekeleza maelekezo ya Waziri Mkuu ambayo aliitaka tume hiyo kuhakikisha inakamilisha ujenzi wa ofisi za tume hizo kwa wakati ili shughuli za uchaguzi za mwaka huu zinafanyika kwenye majengo hayo.

"Kutokana na mkandarasi mpya wa mradi huu ambaye ni SUMA-JKT, tumewahakikishia wanakamati wa PAC kuwa ifikapo Aprili mwaka huu, mradi wa ujenzi wa ofisi za tume utakuwa umefikia hatua kubwa kwa kiwango cha kuruhusu shughuli kuanza kuendeshwa katika majengo haya," alisema.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mkurugenzi wa Uchaguzi NEC, Wilson Mahera, alibainisha kuwa tume hiyo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ardhi na Kampuni ya Ujenzi ya Jeshi la Kujenga Taifa- SUMA JKT CCL, wanaouhakikia Aprili mwaka huu tume itaanza kuendesha shughuli zake kwenye majengo hayo.

# Wenyeviti Bahi watakiwa kusimamia shule shikizi

**Na Augusta Njoji,** BAHI

WENYEVITI wa vijiji wilayani Bahi, wameagizwa kuzisimamia shule shikizi katika maeneo yao ili kuleta matokeo chanya kwa jamii husika.

Shule hizo zimeanzishwa na wananchi ili watoto wao waliofika umri wa kuanza shule wapate elimu kutokana na shule za msingi kuwa mbali na maeneo wanayoishi.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alipotembelea Shule Shikizi ya Lowassa inayohudumia vitongoji vya Nkomango na Mlingeni katika Kijiji cha Mkakatika, wilayani humo.

Munkunda alisema kuwa wenyeviti hao wanapaswa kutambua kuwa shule shikizi katika maeneo yao ni mali ya wananchi wana wajibu wa kuzisimamia ipasavyo katika uendeshaji wake.

"Wajibu wa serikali ni kuleta walimu na pale inapotokea changamoto ya ukosefu wa walimu basi kijiji kina wajibu wa kumtafuta mwalimu wa kujitolea ili awafundishe wanafunzi," alisema.

Alieleza kuwa shule hizo zimeanzishwa kutokana na shule za msingi kuwa mbali na maeneo husika, hivyo wazazi kuhofia usalama wa watoto wao.

Aliwataka viongozi hao kushirikiana na wananchi kuhakikisha mazingira ya wanafunzi kujifunzia yanavutia kusoma katika shule hizo.

"Hadi kufikia Machi 9, mwaka huu mazingira ya shule hizi katika maeneo yenu yawe yameboreshwa vinginevyo wananchi hawakuwa na uhitaji wa kuanzisha shule hizi," alisema.

Awali, mmoja wa wazazi Nyambuya Machela, alimwambia kiongozi huyo kuwa kuanzishwa kwa shule hiyo kwao kumekuwa na manufaa makubwa kwa kuwa Shule ya Msingi Mkakatika ipo umbali wa takriban kilomita 10.

"Hivyo, watoto wanapofikia umri wa kuanza shule wazazi tunaingia hofu kuhusu usalama wao wanapotoka nyumbani kwenda shule na kurudi, lakini shule hii imetusaidia, angalau wanapoanza elimu ya msingi wanaweza kutembea umbali huu,"alisema.

Naye msimamizi wa shule hiyo, Abdul Kivuma, alitoa taarifa kwamba shule hiyo ina wanafunzi 107 ambapo darasa la awali ni 26, la kwanza 48 na la pili 33.

# Askari polisi afukuzwa kazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limemfukuza kazi askari wake, Hussein Yahya Rashid (36) baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kusababisha kifo cha mtuhumiwa wa wizi, Mussa Suleiman.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Awadh Juma Mohamed, alithibitisha jana kufukuzwa kazi kwa askari huyo tangu Novemba 11, mwaka jana.

Alisema kosa la askari huyo ni kumkabidhi mtuhumiwa wa kosa la wizi kwa raia ambao walimshambulia hadi kusababisha kifo chake huko Ziwani Mjini Unguja.

Kamanda huyo alisema askari huyo alitakiwa kumkabidhi mtuhumiwa mbele ya Jeshi la Polisi au kituo chochote ili kupata hifadhi na kusubiri taratibu zingine za upelelezi na kufunguliwa mashtaka.

Alisema siku zote wahalifu wanapotenda makosa kimbilio lao ni vituo vya ulinzi ikiwamo Jeshi la Polisi ambako wanaamini hatua za kisheria zitafuatwa ikiwamo kufunguliwa mashtaka.

"Ni kweli Jeshi la Polisi limemfukuza kazi aliyekuwa askari wake Hussein Yahya Rashid ambaye alimkamata raia anayetuhumiwa na makosa ya wizi. Badala ya kutakiwa kumpeleka katika kituo cha Polisi, alimsalimisha kwa raia wenye hasira na kusababisha kifo chake," alisema.

Kamanda Awadhi aliwataka askari wengine kuzifahamu sheria zinazoliongoza jeshi hilo ambalo linafanya kazi zake kwa mashirikiano makubwa na raia.

Alisema Jeshi la Polisi majukumu yake ni kulinda usalama wa raia ambapo wananchi wanapobaini maisha yao yapo hatarini wanatakiwa kujisalimisha kwa taasisi hiyo kwa hatua nyingine zaidi.

# CCM yaahidi kuwalinda wabunge na wawakilishi waliofanya vizuri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ali Ame, amesema Kamati ya Siasa ya Mkoa itawalinda na kuwatetea viongozi wote wa jimbo wanaojitahidi kupunguza kero za wananchi katika majimbo yao.

Aliyasema hayo juzi wakati akikabidhi mabomba ya kusambaza huduma ya majisafi na salama kwa wananchi wa Kijiji cha Moga, Jimbo la Mkwajuni ambayo yametolewa na mwakilishi wake, Ussi Yahya.

Ame alisema kuwa kamati ya siasa ya mkoa ndiyo yenye dhamana ya kupendekeza wagombea wanaofaa kabla ya kupigiwa kura na wananchi.

Hata hivyo, alisema kamati hiyo haitawalinda wawakilishi, wabunge na madiwani ambao hawajatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM na kutatua kero za wananchi majimboni.

"Hili nalisema wazi kabisa, hatutamlinda wala kumtetea kiongozi yeyote wa jimbo ambaye ameshindwa kutatua kero za wananchi na kutekeleza ahadi alizozitoa. Waache watumie hela, umaarufu na uwenyeji lakini hatutampitisha katika ngazi ya mkoa," alisema.

Alisema huu ni mwaka wa lala salama ambao ni wa uchaguzi mkuu, hivyo ni vyema viongozi wa majimbo kucheza na majimbo yao kwa kutekeleza ahadi walizozitoa.

Mwenyekiti huyo alimpongeza mwakilishi wa jimbo hilo kwa jitihada zake za kutatua kero za wananchi ili kujipatia maendeleo.

"Mcheza kwao hutunzwa hivyo tunakupongeza sana mwakilishi na hata mbunge wa jimbo hili kwa jitihada zenu za kutatua kero za wananchi na kutekeleza ilani ya CCM," alisema.

Pia aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuitunza miundombinu hiyo ya maji ili isihujumiwe na baadhi ya watu wasiopenda maendeleo.

Kwa upande wao, wananchi wa kijiji hicho walisema kukamilika kwa shughuli za usambazaji wa majisafi na salama kutawarahisishia kupata huduma hiyo na kufanya shughuli za kimaendeleo.

Tatu Haji, mmoja wa wananchi wa kijiji hicho, alisema wanatumia muda mwingi kufuata huduma ya majisafi na salama na kushindwa kufanya kazi zingine za kujipatia kipato.

"Tunawapongeza sana viongozi wetu kwa juhudi zao. Tuna imani kuwa mabomba haya yakishasambazwa tutapata huduma ya maji kwa urahisi na wakati mwafaka," alisema Tatu.

Naye Mwakilishi Ussi alisema CCM imetoa viongozi wa majimbo na kupata ridhaa ya wananchi ambapo wakati anaomba ridhaa ya wananchi kuwa mwakilishi wa jimbo hilo mwaka 2015 aliahidi kutatua kero ya maji.



Kinamama wa Kijiji cha Chutama, Jimbo la Mkwajuni, Mkoa wa Kusini Unguja, wakiandaa chakula kwa ajili ya vijana waliojitolea kujenga bure jengo la tawi la CCM la kijijini hapo, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watu 496 wanaswa na dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATUHUMIWA 496 wa dawa za kulevya wamekatwa na Jeshi la Polisi kwa kipindi cha mwaka jana, wakiwamo wanawake 17.

Watu hao walikamatwa wakiwa wanasafirikisha, kusambaza, kuuza na kutumia dawa hizo.

Akitoa juzi matukio ya mwaka kwa waandishi wa habari makao makuu ya Polisi Zanzibar, Kilimaji Mjini Unguja, Kamishna wa Polisi Zanzibar, Muhamed Haji Hassan, alisema dawa zilizokamatwa ni Cocaine gramu 806.65, Heroine kilogramu 10 na gramu 806.102.

Alisema bangi ilikamatwa ikiwa na uzito wa kilogramu 659.6 na mirungi iliyokamatwa ilikuwa na uzito wa kilogramu 10.6 pamoja na vidonge vya valium gramu 10.30. "Hata hivyo kuna mwendelezo wa jambo hili. Kuanzia Januari Mosi, mwaka huu, Polisi Zanzibar kwa kushirikiana na Makao Makuu ya Polisi Dodoma, tunaendesha operesheni maalum na tumefanikiwa kuwakamata watuhumiwa wengine 10," alisema.

Kamishna Muhamed alisema miongoni mwa watuhumiwa hao, watatu wanajihusisha na uuzaji wa dawa za kulevya na saba ni watumiaji na pia kete mbili za heroine zilikamatwa, kete tatu na nyongo na 10 za bangi.

Aidha, alisema kutokana na kuwapo kwa tatizo la biashara haramu ya dawa ya kulevya, Jeshi la Polisi Zanzibar kwa kushirikiana na taasisi zingine za ulinzi na usalama, wamejipanga kimkakati kukabiliana na janga hilo.

Kwa mujibu wa kamishna huyo, mikoa yote imeshapewa maelekezo ya kujipanga na kuendeleza mapambano. Pia alisema masheha katika shehia zao wameshaelekezwa kuwasilisha kwa siri taarifa za wauzaji, wasambazaji na watumiaji wa dawa hizo kwa maofisa wa intelijensia waliopangwa katika shehia zao. Kuhusu matukio ya usalama wa barabarani kwa mwaka jana, alisema takwimu za ajali za barabarani zinaonyesha kupungua kwa makosa hayo kwa mwaka huo ikilinganishwa na mwaka 2018.

Alisema kwa mwaka 2019, ajali zilikuwa 311, huku vifo vikiwa 162 na waliojeruhiwa ni 405 ikilinganishwa na mwaka 2018 ajali zilikuwa 319, vifo 163 na majeruhi 584.

"Kutokana na takwimu hizo kuna upungufu wa ajali nane sawa na asilimia mbili na mwaka 2019 kulikuwa na upungufu wa kifo kimoja huku majeruhi wakiwa 179 nao wamepungua sawa na asilimia 30," alisema.

# Wafanyabiashara wahimizwa kutumia mfumo utoaji taarifa

**Na Sabato Kasika**

WAFANYABIASHARA nchini wamehimizwa kutumia mfumo wa utoaji taarifa za kibiashara uliomo kwenye Dirisha la Taifa la Biashara.

Lengo la kutumia mfumo huo ni kutaka wafahamu taratibu za usafirishaji nje ya nchi, uingizaji na upitishaji wa mazao na bidhaa mbalimbali nchini.

Msisitizo huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Leseni wa Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Andrew Mkapa, alipokuwa akizungumza katika mahojiano maalumu. "Mtu anapoingia kwenye mfumo huo, anaweza kuona taarifa za hatua kwa hatua, ambazo mfanyabiashara anapaswa kuzipitia na kuzifuata, ili kupata leseni na vibali vinavyohitajika kutoka taasisi mbalimbali kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi, kuingiza au kupitisha nchini bidhaa na mazao mbalimbali," alisema Mkapa.

Mkurugenzi huyo alitolea mfano Tanzania kuwa wameshaweka taarifa hizo zinazohusiana na usafirishaji nje ya nchi wa mazao makuu ya kimkakati kama kahawa, pamba, korosho na mengine kadhaa.

"Taarifa hizo pia zinahusu uingizaji nchini wa dawa, vipodozi, vifaa tiba, magari na vingine...mfanyabiashara akiingia kwenye mfumo huo, anaweza kuona ni hatua gani na ngapi anapaswa kupitia," alisema.

Mkapa alisema kupitia mfumo huo, mfanyabiashara pia atajua ni vibali au leseni gani anatakiwa kuwa nayo ili kusafirisha nje ya nchi, kuingiza ndani au kupitisha nchini bidhaa hizo kwenda kwingine.

Alisema, mfumo huo utasaidia kurahisisha ufanyaji biashara nchini, pia upatikanaji wa taarifa hizo kwa wafanyabiashara kutoka nchi nyingine, ambao wangependa kufanya biashara nchini.

"Uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini ni pamoja na kupunguza muda, gharama, pia inapobidi kupunguza sheria na kanuni mbalimbali, ambazo zinaonekana si za lazima, ni kikwazo katika ufanyaji biashara," alisema.

Alisema, mfanyabiashara anapozifahamu taratibu hizo kabla, zitamsaidia na kumpa nafasi ya kujiandaa kuzitekeleza bila kupoteza muda mwingi wa kuzunguka na kuzitafuta kwanza," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Tiba wa Hospitali ya Rufani ya Kilutheri ya Haydom, iliyopo Mbulu mkoani Manyara, Dk. Emanuel Nuwas (kulia), akitoa maelezo kwa Mwakilishi wa Balozi wa Norway hapa nchini, Elizabeth Jacobsen (kushoto), kuhusu utendaji wa mashine ya uchunguzi ya CT Scan, iliyofungwa hospitalini hapo, baada ya kuzinduliwa juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Barabara yawa kikwazo kwa wanavijiji

**Na Julieth Mkireri**, KIBAHA

WAKAZI wa Kitongoji cha Waya, Kijiji cha Waya Kata ya Kwala, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, wanakabiliwa na changamoto ya ubovu wa barabara, hali inayopelekea wanafunzi kushindwa kufika shule kipindi cha mvua.

Diwani wa Viti Maalumu, Josephine Gunda, alibainisha hayo wakati akizungumza na Nipashe.

Gunda alisema barabara hiyo kipindi cha mvua imekuwa inajaa maji, kutokana na kuwa karibu na mito miwili, na hivyo wanafunzi kushindwa kuvuka. Aidha, alisema, kutokana na hali hiyo, waliisemea kwenye vikao vya Baraza la Madiwani, ambapo katika bajeti ya Wakala wa Barabara za Vijjini na Mjini (TARURA) mwaka 2019/2020 imepangwa kufanyiwa ukarabati.

Gunda anasema kuwa mbali ya changamoto ya barabara, pia wanafunzi wanaotoka katika Kijiji cha Waya, wamekuwa sugu kwa utoro kutokana na umbali.

"Wanafunzi wanaotoka Kijiji cha Waya wanalazimika kutembea umbali wa kilomita zaidi ya nne kila siku, kutoka kijijini hapo hadi Kwala, wanashindwa kumudu umbali huo na kupumzika katikati ya siku za masomo," alisema.

Diwani huyo anaeleza kuwa kwa sasa wameanza ujenzi wa madarasa katika kijiji hicho, ili kunusuru watoto hao ambao wamekuwa na ufaulu hafifu.

"Kuna shule ya miti tuliijenga ili watoto wa darasa la kwanza na la pili waanze kusoma, tulifanya hivyo na sasa kuna darasa moja kwa kiwango cha tofali tunalimalizia, wanasoma wakiingia darasa la tatu wanahamia Shule ya Kwala, tumeomba halmashauri na idara ya elimu kusajili shule hii ambayo tunaamini itakuwa mkombozi kwao," anaeleza Gunda.

Diwani pia alizungumzia, mwamko mdogo kwa watoto wa wafugaji, hali inayosababisha mara kwa mara kushika nafasi za mwisho kwenye ufaulu.

Alisema jamii ya wafugaji wamekuwa wakihama hama maeneo na watoto wao, wakati mwingine hawaonekani hadi inapofikia kipindi cha mitihani na hivyo kusababisha kutofanya vizuri kwenye matokeo ya kitaifa.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa jamii hiyo kuthamini elimu na kuwapa nafasi watoto kwenda shule.

# Wakimbia nyumbani kukwepa kukeketwa

**Na Sabato Kasika**

WASICHANA 36 wameokolewa dhidi ya vitendo vya ukeketaji baada ya kukimbilia, katika kituo cha nyumba salama cha Butiama kinachomilikiwa na Shirika lisilo la Kiserikali la Hope for Girls and Women Tanzania.

Wasichana hao walikimbia kutoka nyumbani kwao Tarime, mkoani Mara Desemba mwaka jana kuepuka kukeketwa na wazazi wao na kwenda kwa wasamaria wema waliowasafirisha hadi katika nyumba hiyo.

Akizungumza jana na gazeti hili kwa njia ya simu, Mkurugenzi wa Asasi isiyo ya Kiserikali ya Hope for Girls and Women Tanzania, Rhobi Samwelly, alisema tayari wasichana 27 wamerudi kwa wazazi wao tangu mwanzoni mwa mwezi huu.

"Yaani ni kwamba baada ya kuwapokea watoto, tulishirikisha ustawi wa jamii, dawati la jinsia na kisha tukaenda kwa wazazi wao kujenga urafiki na kuwaelimisha kuhusu madhara ya ukeketaji," alisema Rhobi.

Alifafanua kuwa wazazi 27 walikubaliana na elimu na hiyo na kuahidi kuachana na mpango wa kuwakeketa, kisha ukaandaliwa utaratibu maalum wa kuwarejesha wasichana hao nyumbani kwao ili waendelee na masomo.

"Tuna fomu maalum ambazo mzazi anazijaza akiahidi kutomfanyia mtoto wake vitendo vya ukatili, vinginevyo achukuliwe hatua za kisheria, na pia inasainiwa na sisi, ustawi wa jamii na dawati la jinsia," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema, wasichana wengine tisa wataendelea kuwapo kwenye kituo hicho baada ya wazazi wao kukataa kuwapokea, wakidai kwamba mabinti hao wamewadhalilisha kwa kukataa kukeketwa.

"Sisi tutaendelea kuwa nao na tutawasomesha wale, ambao bado wako shule za msingi na waliokuwa wamehitimu na hawakufaulu, watapata mafunzo maaluma ya kuwawezesha kujitegemea hapo baadaye," alisema.

Aidha, alisema, Hope for Girls and Women Tanzania, ina makao makuu yake mjini Mugumu Serengeti, lakini ina marafiki karibu kila kona ya mkoa wa mara, hivyo marafiki hao ndiyo waliosaidia kuokolewa kwa wasichana hao.

Alisema, Desemba ya kila mwaka huwa kuna shughuli za ukeketaji kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa wa Mara na hasa Tarime na Serengeti, hivyo mwezi ulipotimia tu wakakimbia ili wasikeketwe.

"Tuna marafiki kila kona, na ilikuwa rahisi kwao kwenda kwa marafiki zetu hao, ambao waliwasafirisha hadi kwetu na tukafanya kila njia ya kuwawezesha kurudi kwa wazazi, lakini baada ya kuhakikishiwa usalama wao," alisema.

# Rais awageuzia kibao wanajeshi kisa ndege

**TEHRAN, Iran**

RAIS wa Iran, Hassan Rouhani, amesema kuwa majeshi ya nchi hiyo lazima yaeleze jinsi ilivyodungua kimakosa ndege ya abiria ya Ukraine wiki iliyopita.

Naye, Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo, Mohammad Javad Zarif alikiri kuwa raia wa Iran walidanganywa kwa siku kadhaa baada ya ajali hiyo.

Alisema kuwa yeye na Rais Rouhani hawakufahamishwa kuhusu tukio hilo.

Majeshi ya Ulinzi ya Iran yaliwaua watu 176 wakati ilipodungua "kimakosa" ndege ya Ukraine wakati nchi hiyo ilipozozana na Marekani kufuatia mauaji ya Jenerali Qasim Solemani.

Saa kadhaa kabla ya ajali hiyo, Iran ilishambulia kwa makombora ya masafa ya mbali vituo viwili vya vikosi vya Marekani nchini Iraq.

Akizungumza katika runinga ya kitaifa juzi, Rais Rouhani alitaka jeshi hilo kuangazia hatua ya pili ya uchunguzi kwa makini

kitu cha kwanza nikuwaambia watu ukweli.

"Watu wanaomboleza watafarijika wakijua kwamba tunawawajibisha waliosababisha ajali hiyo kwa kusema nao na kuwaambia ukweli," alisema Rais Rouhani.


Aidha, Rais Rouhani alitoa wito kwa kikosi hicho kuwaelezea watu kile kilichofanyika tangu ajali hiyo ilipotokea.

Akiwa ziarani nchini India Zarif, alisema katika mahojiano na kituo kimoja cha televisheni kuwa: "Mimi na rais hatukujua ni nini kiliangusha ndege hiyo na punde tulipobaini, tulitoa maelezo".

Alisifu wanajeshi wa nchi hiyo kwa kukiri makosa. Hata hivyo, wakosoaji walishangaa kwanini iliwachukua siku tatu kukiri makosa hayo hadi pale mataifa ya magharibi yaliposema yana ushahidi wa kuthibitisha ndege hiyo ilidunguliwa na makombora ya Iran.

Kanda ya video iliyothibitishwa na gazeti la New York Times ilionyesha jinsi makombora yalivyokuwa yakipita katika anga la Tehran na baadaye kulipuka ilipokutana na ndege.

*BBC*



Wagombea urais wa Chama cha Demokrati kutoka kushoto Bilionea Tom Steyer, Seneta Elizabeth Warren, Makamu wa Rais wa zamani, Joe Biden, Seneta Bernie Sanders, Meya wa zamani Peter Buttigieg na Seneta Amy Klobuchar wakiwa katika mdahalo, Marekani. **PICHA: REUTERS**

# Misri, Ethiopia, Sudan zakubaliana kuhusu Mto Nile

**ADDSIS ABABA, Ethiopia**

NCHI za Misri, Ethiopia na Sudan zimefikia makubaliano ya awali ya kujaza maji na shughuli nyingine kwenye bwawa kubwa linalojengwa Mto Nile.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa na nchi hizo pamoja na Marekani na Benki ya Dunia (WB), imesema kwamba washiriki wanaojadiliana wamekubaliana kujaza bwawa la Grand Renaissance linalojengwa Ethiopia wakati wa msimu mvua kati ya miezi ya Julai na Agosti.

Hata hivyo, taarifa hiyo haikusema lolote kuhusu masuala ya msingi yanayozunguka mgogoro huo ambayo ni kasi ya kujaza bwawa hilo.

Ethiopia inataka kujaza bwawa la Grand Renaissance kwa miaka sita lakini Misri imependekeza angalau mradi huo uchukue kipindi cha miaka 10 kwa kuhofia kwamba kuchukua kipindi kifupi kutaathiri mtiririko wa maji ya Mto Nile ambayo inategemea asilimia 90 ya maji ya mto huo.

Makubaliano ya mwisho yatatiwa saini Januari 28-29, wakati ambapo mawaziri kutoka nchi tatu watakuwa wanakutana mjini Washington Marekani.

Makubaliano ya awali ambayo yalifikiwa na Waziri wa Fedha wa Marekani na Rais wa WB yalitia maanani mahitaji ya Ethiopia ya kuanza uzalishaji wa umeme mapema.

Lakini pia yanazungumzia hatua za kupunguza athari kwa Misri na Sudan iwapo kutakuwa na vipindi virefu vya kiangazi katika nchi hizo zilizopo kwenye mkondo wa maji ya Mto Nile.

Kufikiwa kwa makubaliano hayo kunapunguza wasiwasi uliokuwapo kati ya Ethiopia na Misri ambazo zimekuwa zikizozana tangu Ethiopia ilipoanza kujenga bwawa hilo mwaka 2011.

Ujenzi wa Bwawa la Grand Renaissance linalojengwa Ethiopia ukishamalizika, mradi huo unaogharimu kima cha Dola za Marekani bilioni 5, litakuwa ndio bwawa kubwa zaidi la uzalishaji umeme barani Afrika lenye uwezo wa megawati 6,000.

*BBC*

# Spika aomba msaada nchi za Kiarabu

**TRIPOL, Libya**

SPIKA wa Bunge la Libya, Aguila Saleh, akiwa ziarani jijini Cairo Misri amedhuru Bunge la Jumuiya ya nchi za Kiarabu.

Akiwa nchini humo, alithibitisha kwamba vikosi vinavyoongozwa na Marshal Khalifa Haftar, vinaendeleza harakati zao na muda wowote vitaingia mjini Tripoli.

Pia, alitoa wito kwa nchi za Kiarabu kutotambua tena Serikali ya Umoja wa Kitaifa ya Tripoli inayoongozwa na Fayez el-Sarraj.

Vilevile, alitoa wito kwa nchi za Kiarabu kuingilia kati ili kukabiliana na Uturuki ambayo imeingilia kijeshi nchini Libya.

Aguila Saleh amebaini kwamba mikataba miwili iliyotiliwa saini kati ya Ankara na serikali ya Fayez el-Sarraj ni kinyume cha sheria, kwani hawajapata idhini ya Bunge.

Katika taarifa, Bunge la Jumuiya ya nchi za Kiarabu limelaani uamuzi wa Uturuki wa kupeleka vikosi nchini Libya.

Wakati huohuo, baada ya kushindikana kwa mazungumzo jijini Moscow, nchini Urusi, Ujerumani inatarajia kuwa mwenyeji wa mkutano wa kimataifa Januari 19 ili pande husika zisitishe mapigano nchini Libya na kuzindua tena mchakato huo.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya mvutano unaendelea kutokea mji mkuu wa Libya Tripoli.

Hata hivyo, hali ya utulivu inaendelea kutawala jijini Tripoli kila upande unajaribu kushikilia msimamo wake licha ya ukiukaji katika makubaliano ya kusitisha mapigano.

Kambi ya Khalifa Haftar imeongeza vikosi vyake katika maeneo inayoshikilia, wakati vikosi vya Fayez el-Sarraj vinaendelea kutegemea msaada wa mamluki kutoka Syria, waliotumwa na Uturuki kusaidia serikali ya Tripoli.

Wapiganaji 2,000 kutoka Syria waliwasili jijini Tripoli katika wiki za hivi karibuni.

**RFI**

**Wakati huohuo, baada ya kushindikana kwa mazungumzo jijini Moscow, nchini Urusi, Ujerumani inatarajia kuwa mwenyeji wa mkutano wa kimataifa Januari 19 ili pande husika zisitishe mapigano nchini Libya na kuzindua tena mchakato huo.**

# Mbunge wa Chadema amjibu Freeman Mbowe

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Rombo, Joseph Selasini (Chadema), amemjibu Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Freeman Mbowe, kuwa hana siri yoyote iliyomsukuma kuchukua uamuzi wa kujiuzulu nafasi ya unadhimu wa upinzani bungeni.

Amesema uamuzi huo ameuchukua kutokana na utashi wake binafsi na kwamba hana mpango wowote wa kukihama chama hicho.

Selasini alisema jana kuwa yeye si mwoga katika kufanya uamuzi unaohusu mambo yake binafsi au jamii inayomzunguka kwa kuwa amekuwa kiongozi kwa muda mrefu na hivyo kuwa na uzoefu wa kutosha kuhusu masuala ya uongozi.

"Nadhani mmesikia 'comment' (maelezo) yake kuwa nina mambo yangu ya siri, mimi nipo kwenye mageuzi kabla ya Mwenyekiti Mbowe, yeye ameingia kwenye mageuzi baada ya Sheria ya Vyama vya Siasa kutungwa na Chadema kuzaliwa, mimi nipo kwenye mageuzi tangu miaka ya tisini (1990)," Selasini alitamba.

Mwanzoni mwa wiki, Selasini aliandika barua kwenda kwa Mbowe, akieleza kujiuzulu nafasi ya unadhimu wa upinzani bungeni baada ya kukaimu nafasi hiyo kwa miaka miwili bila kupewa barua rasmi ya kushika nafasi hiyo.

Hata hivyo, uamuzi wake huo ulikosolewa vikali na kiongozi wake wa chama, Mbowe, ambaye alieleza kushangazwa na mbunge huyo mzoefu akimtaka asema kama ana jambo la siri.

"Kama hakupewa barua ya kuteuliwa, amewezaje kuandika barua ya kujiuzulu? Kama amefanya kazi zake vizuri, wabunge wote wanamheshimu, wanamsikiliza, uongozi wa Bunge unampa ushirikiano kwa miaka miwili, sasa anashindwaje kumalizia miezi minne iliyobaki?" Mbowe alihoji.

Jana, Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa (Chadema), pia alizungumzia suala hilo, akidai Selasini hajawahi kufikisha kwenye chama malalamiko ya kubughudhiwa na Ofisi ya Spika kutokana na kukosa barua ya kutambulishwa kukaimu nafasi hiyo.

Selasini alikaimu nafasi hiyo baada ya Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, kupelekwa nje ya nchi kupata matibabu ya kibingwa baada ya kushambuliwa kwa kupigwa risasi Septemba 7, 2017.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, akitokea nchini Msumbiji, ambako alimwakilisha Rais John Magufuli, kwenye uapisho wa Rais wa Msumbiji Filipe Nyusi. Kushoto ni Rais mstaafu wa Awamu ya Pili, Benjamin Mkapa, ambaye alikuwapo katika msafara huo. **PICHA: OWM**

# Waziri aagiza mkandarasi kulipwa mil. 300/- za maji

**Na Steven William,** MUHEZA

NAIBU Waziri wa Maji, Juma Aweso, amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Kitila Mkumbo, kutenga Sh. milioni 300 za kumlipa mkandarasi anayejenga mradi mkubwa wa maji kutoa maji kutoka mji wa Pongwe kupeleka Muheza ambao umefikia asilimia 95.

Aweso aliyasema hayo juzi mbele ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, katika mkutano uliofanyika katika ukumbi wa Tate Plus mjini hapa.

Naibu Waziri huyo alisema serikali inajenga mradi wa maji kutoka Pongwe jijini Tanga hadi Muheza Mjini, lakini umechelewa kutokana na mkandarasi alikuwa anadai zaidi ya Sh. milioni 700 amelipwa Sh. milioni 270 tu.

Kutokana na hali hiyo, alisema amemwagiza Katibu Mkuu wa Wizara kutafuta fedha Sh. milioni 300 kwa ajili ya kulipwa mkandarasi huyo ili aendelee na kumalizia kazi hiyo na hatimaye wananchi wa Muheza wapate maji safi na salama ambayo ni kero ya muda mrefu. Meneja wa Wakala wa Majisafi na Salama Wilaya ya Muheza, Elikana Kayungiro, alisema mradi huo utawanufaisha wananchi 15,000 ambao wanakabiliwa na tatizo la maji kwa miaka mingi.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru, alisema lazima mkandarasi anayejenga mradi wa maji alipwe mara moja ili kazi hiyo ifanyike kwa haraka.

Alisema mkandarasi amefanya kazi mpaka kufikia asilimia 95 ya mradi na anadai zaidi ya Sh. milioni 700, hivyo kuagiza apewe kiasi kilichotengwa haraka.

Kuhusu ujenzi wa barabara kwa kiwango cha Lami yenye urefu wa kilomita saba kutoka Muheza mjini mpaka Bombani, aliagiza ijengwe mpaka tarafa ya Amani urefu wa kilomita 35.

Katibu mkuu huyo alifanya mikutano katika wilaya za Handeni, Kilindi, Korogwe, Lushoto. Pangani, Muheza na Tanga.

katika hatua nyingine, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema serikali imetoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya ya Muheza.

Pia alisema Sh. milioni 400 zimetolewa na serikali kwa ajili ya kupanua Kituo cha Afya cha Mkuzi na sasa itapeleka fedha zingine kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Misalai, Tarafa ya Amani.

Alisema katika Kituo cha Afya cha Mkuzi, wataanza kutoa huduma ya upasuaji ili kuwezesha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo kupata huduma hiyo karibu badala ya kusafiri umbali mrefu hadi Muheza mjini kwenye Hospitali Teule ya Wilaya.

Waziri pia alisema wananchi wanaoishi Tarafa ya Amani wana changamoto kubwa ya kufika Muheza mjini kutokana na umbali, hivyo serikali itapeleka gari ya kubeba wagonjwa ambalo alisema kwa sasa liko baharini.

# Hydom yapata vifaa vya kisasa

**Na Godfrey Mushi,** MBULU

HOSPITALI ya Rufani ya Kilutheri ya Haydom iliyoko Mbulu mkoani Manyara, imeanza kutoa rasmi huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali kwa kutumia vipimo vya CT Scan na 'Digital X-Ray'.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, jana alizindua vifaa vipya vya tiba ukiwamo mtambo mpya wa kuzalisha hewa ya Oksijeni na mtambo wa kuchoma taka hatarishi vilivyoigharimu hospitali hiyo zaidi ya Sh. bilioni 1.6.

Katika uzinduzi huo, Waziri Mwalimu aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga.

Kabla ya uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Emanuel Nuwass, alimweleza waziri huyo kuwa kuanzia sasa wagonjwa wanaotaka huduma hiyo watapata vipimo ndani ya hospitali hiyo.

"Kuanzia sasa wagonjwa wanaohitaji vipimo vya CT Scan hawatalazimika kwenda mikoa mingine na kutumia gharama kubwa za usafiri. Tumewekeza fedha nyingi kuleta vifaa hivi na sasa ndoto yetu imekamilika. huduma zetu zitakuwa bora zaidi," alisema Dk. Nuwass.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, mashine hiyo ya CT Scan mpaka sasa tayari imeshahudumia wagonjwa 250 baada ya kununuliwa kutoka Kampuni ya Siemens kwa thamani ya Sh. milioni 654.2

Mashine ya pili ni Digital X-ray iliyonunuliwa kutoka Kampuni ya GE Healthcare imegharimu Sh. milioni 320.2

Dk. Nuwass aliitaja mashine ya tatu iliyonunuliwa ili kuboresha huduma za tiba hospitalini hapo ni pamoja na mtambo wa kuzalisha hewa ya oksijeni.

"Mtambo huu wa kuzalisha hewa ya oxygen mpaka sasa umeshaokoa Sh. milioni 74 kwa muda wa miezi minne kama tungenunua kutoka sehemu nyingine. Katika kuboresha huduma, moja ya vitu muhimu ni miundombinu bora na wezeshi hasa vifaa tiba," alisema.

Baada ya maelezo hayo, Waziri alisema hivi sasa serikali inasubiri mapendekezo rasmi ya uongozi wa mkoa wa Manyara na Hospitali ya Kilutheri ya Haydom ya kutaka kupandishwa hadhi kuwa hospitali ya rufani ya serikali.

"Katika hospitali zinazonifurahisha katika ukanda huu wa kaskazini, niseme ukweli ni Hospitali ya Kilutheri ya Haydom. Niandikieni mapendekezo yenu ya kutaka kupandishwa hadhi kuwa hospitali ya rufani na mimi nitabariki," alisema.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL.**

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu:**0714404491/0746995144**


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**


### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI


**KASIBANTE FM RADIO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki, yenye Namba **MC 361 AMJ, chasis No. KEFKE700017660, Engine No. 156FM12D5176970.** Kadi ilipotea, na aliripoti kituo cha polisi cha Bukoba tarehe1/1/2020 na kupewa No: KAG/BUK/RB/20807/2020.

Kwa yeyote atakayeiona aipeleke kituo cha polisi kilichoko karibu naye.

Au awasiliane naye.
**No: 0767 814844.**

115588602

### KUPOTEA KWA VYETI



**GEORGE GREGORY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1244-0037 kilichotolewa na MOYOWOSI SEKONDARI mwaka 2007. Cheti cha Tanganyika Medical Training Board Nursing chenye namba 19961, Enrollment Certificate Midwife chenye namba 47737, Enrollment Certificate of Nursing chenye namba 58047 vilivyotolewa na KIBONDO SCHOOL OF NURSING mwaka 2015.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi: KAS/RB/1047/2019.**

215587902

### KUPOTELEWA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KARIMU JUMA MSUYA**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki
MC 657 AHK,

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

Polisi Taafifa :

MWG/RB/KF/172/2018

115588502

### KUPOTEA KWA KADI

EVA BAMBA SAKASA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 862 ACY RAV 4. Chassis namba JTEHH20V900105361. Engine namba 1AZ0332429. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DAR/KIJ/RB/49476/2020.

215588302

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SWETU THABIT FUNDIKILA** anatangaza kuunguliwa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T430 ATD** MITSUBISH FUSO. Chasis **No FH217C503496.** Engene **No 6D16862965.** Taarifa yoyote itolewe kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **IR/TR/RB/86/2020.**

115587702

### TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

Wamiliki wa kampuni ya **Luminant Electrical Contractors Co. Limited** (yenye namba za usajili **141423 ya 14/3/2018**) wanapenda kuutangazia umma kuwa kampuni yao haikuweza kufanikiwa kuanzisha biashara kama ilivyokua matarajio yao hivyo kuamua kuifunga kampuni kwa hiari.

115587802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No; 13/2020
Ombi la VENANCIA PETER SANIEL Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu PETER SANIEL MGHAMBA
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/02/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/01/2020

115588002

**AMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**

MAHAKAMA YA MWANZO YA (W) YA IRINGA MJINI
WILAYA YA IRINGA
SHAURI LA NDOA NA 1/2020

MDAI; WILLIAM MLIGO
MDAIWA; JACKLINE PAUL MLULA LUHOTA

KWA KUWA MDAI AMELETA MADAI YAKE YA KUACHANA NA MDAIWA. KWAHIYO UNAHITAJIKA UNAHITAJIKA KUHUDHURIA BINAFSI KATIKA TAREHE 30/1/2020SAA 2:30 ASUBUHI KWA KUJIBU DAI HILO. KWAKUWA SIKU HIYO YA KUKATWA SHAURI HILO NI LAZIMA KULETA MASHAHIDI WENU NA HATI ZOTE ZINZOHUSU SHAURI HILO KWAAJILI YA KUJITETEA KATIKA SHAURI HILO.

USIPOFIKA SHAURI LITASIKILIZWA UPANDE MMOJA.

HATI HII IMETOLEWA LEO 14/1/2020

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI

115588102


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Nipashe

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**NJOO UTANGAZE**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# TUCHEL: ICARDI ANANIKUNA SANA




**PARIS,** Ufaransa

THOMAS Tuchel amesema alikuwa na "furaha kubwa" kwa Mauro Icardi baada ya Paris Saint-Germain kupata ushindi mtamu dhidi ya Monaco, juzi Jumatano.

Icardi alitolewa benchi kipindi cha pili kwenye ushindi huo wa mabao 4-1, ambapo Kylian Mbappe alifunga mara mbili na Neymar akafungwa kwa penalti, huku Pablo Sarabia naye akitikisa nyavu.

Lakini Tuchel alimsifia fowadi huyo, ambaye amefunga mabao 17 kwenye mechi 21 kwa kipindi chake anachocheza kwa mkopo hapo akitoka Inter Milan.

"Aligusa mipira michache kwenye dakika chache mchezoni. Tuna Angel (Di Maria), Neymar, Kylian ambaye anagusa mipira mingi, hivyo ni mchanganyiko mzuri," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Mauro anafanya kazi na sisi, akicheza kwa staili nzuri na nidhamu ya hali ya juu pamoja na wachezaji wenzake jambo ambalo ni muhimu kwetu.

"Sasa hajafunga katika mechi zake mbili zilizopita, lakini anacheza kwa nidhamu ya hali ya juu. Lilikuwa jambo muhimu na kuvutia. Sina shaka na Mauro.

"Tuliamua kuwaacha Kylian na Neymar kama washambuliaji kwa dakika 70, lakini nina furaha kubwa na Mauro."

# Sarri aumia Messi kumzidi Ronaldo

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri amesema "kwa uhakika inatia hasira" kwamba mtu mmoja ameshinda Ballon d'Or mara nyingi zaidi kuliko nyota, Cristiano Ronaldo.

Nyota wa Barcelona, Lionel Messi alimshinda Ronaldo kwa Ballon d'Or moja zaidi na kuweka rekodi ya kutwaa mara sita Desemba mwaka jana.

Matokeo ambayo yalikuja licha ya Ronaldo kuisaidia Juve kutwaa taji la nane mfululizo la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na raia huyo wa Ureno alishinda pia taji la Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Sari anaona kwamba Ronaldo – ambaye aliukosa mchezo wa Jumatano wa ushindi wa mabao 4-0 wa Coppa Italia hatua ya 16-bora dhidi ya Udinese kutokana na kuumwa – anaweza kuongeza Ballon d'Or ya sita na kuwa sawa na Messi.

"Ningependa kumsaidia kwanza Cristiano kushinda Ballon d'Or ya sita," alisema Sarri akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa uhakika inatia hasira kufikiria kwamba kuna mtu ameshinda (Ballon d'Or) nyingi kuliko yeye.

"Namfikiria yeye na nafikiria kumsaidia yeye na hiyo ndiyo dhamira yangu na nafikiri kumsaidi yeye ni jambo la maana kabisa.

"(Paulo) Dybala atakuwa mmoja wa wanaowania tuzo hiyo kwa miaka michache ijayo, nafikiri hivyo."

Huku Ronaldo akiwa amekaa nje ya dimba, mshambuliaji huyo wa Juve, Dybala alifunga mara mbili na kuiwezesha Juve kuikarisha Udinese.





# *Kocha Milan afurahia usajili wa Ibrahimovic*

**MILAN,** Italia

KOCHA wa AC Milan, Stefano Pioli amesema kumsajili Zlatan Ibrahimovic imekuwa ni "muhimu sana" kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Ibrahimovic amerudi kwenye kikosi cha Milan kwa mara ya pili baada ya kuwa na Rossoneri hao ambapo alitwaa taji la Ligi Kuu, Scudetto, msimu wa 2010-11, baada ya kumaliza muda wake kule katika klabu ya LA Galaxy ya Marekani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 38, alianza kwenye mchezo wake na Milan kwa kufunga bao wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Cagliari wiki iliyopita.

"Kumsajili Ibrahimovic kwa hakika limekuwa jambo muhimu sana," alisema Pioli akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa uhakika ni jambo muhimu kwa upande wetu, kuliko kile anachokifanya kila siku dimbani, na hata alichokifanya dhidi ya Cagliari.

"Ibra atatuimarisha sisi kufikia malengo yetu. Ni mchezaji wa kiwango cha juu anaweza kuisaidia timu kwa sababu anafunga mabao mazuri na ya muhimu kwa upande wetu.

# Arteta atishia Arsenal kuisusia safari ya Dubai

**LONDON,** England

MIKEL Arteta atafuta safari ya Arsenal ya muda mfupi Dubai kama ataona kuwa hakuna usalama kwa klabu hiyo kwenda huko Mashariki ya Kati.

Huku Ligi ya England ikitarajiwa kuwa na mapumziko mafupi kwa msimu huu 2019-20, Arsenal imepanga kuweka kambi ya mazoezi ya siku nne kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu wa Februari 16 dhidi ya Newcastle United.

Lakini timu nyingine kama Manchester United imefuta safari yake ya uwezekano wa kwenda Qatar kutokana na kutokuwa na utulivu wa kisiasa.

"Arsenal itafanyia kazi kuangalia uwezekano wa safari hiyo, kabla ya klabu kuruhusiwa kwenda.

"Suala la usalama ndio kitakuwa kipaumbele chetu.

"Kama itashauriwa na watu wanaofanya maamuzi kwamba haifai kufanya safari hiyo, hatutakwenda kokote.

"Tumezungumzia kuhusu maeneo mbalimbali na tutaangalia wapi panatufaa, lakini kote huko usalama ndio jambo la msingi zaidi," alisema kocha Arteta akiwaambia waandishi wa habari.





# KOULIBALY ADAIWA KUMALIZANA NA UNITED

**MANCHESTER,** England

KWA mujibu wa gazeti la Daily Mail, klabu ya Manchester United imedaiwa kukamilisha usajili wa beki wa kati wa Napoli, Kalidou Koulibaly kwa ada ya pauni milioni 60.

Koulibaly alikuwa akihusishwa pia na Tottenham na Arsenal, lakini kwa mujibu wa Daily Mail na taarifa za kutoka Italia, Man United imefanya haraka kuinasa saini yake.

Hata hivyo, beki huyo hatajiunga na timu yake mpya Januari, atasubiri hadi mwishoni mwa msimu, huku saini yake ikidaiwa itakuwa kitu muhimu kwenye kuimarisha beki ya wababe hao wa Old Trafford.

Mwandishi wa habari wa Italia, Fabio Santini amefichua taarifa hizo alipozungumza kwenye kipindi cha televisheni cha Il Processo aliposema Napoli itampiga bei Koulibaly kwenda Man United kwa ada ya kati ya euro milioni 70.

Kwa muda mrefu sasa mashabiki Man United wamekuwa wakihitaji beki mwingine wa kati wa kiwango cha dunia kwenda kuungana na beki wao, Harry Maguire.

# *Rashford apambaniwa afya aivae Liverpool*

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United itafanya kila "kitu kiwezekanacho" kuhakikisha Marcus Rashford anakuwa fiti kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu kuwavaa vinara, Liverpool Jumapili, kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer amesema.

Rashford aliingia wakati United ikishinda 1-0 kwenye mchezo wa raundi ya tatu wa Kombe la FA dhidi ya Wolves pale Old Trafford, lakini alicheza kwa dakika 16 tu kabla ya kutolewa nje baada ya kuumia mgongo kwa kufanyiwa faulo na Matt Doherty, juzi Jumatano.

Ingawa Rashford alikuwa dimbani wakati Juan Mata alipofunga bao la ushindi, Solskjaer ameeleza maamuzi ya kutaka kuhakikisha mchezaji huyo anakuwa fiti kabla ya kwenda pale Anfield.

Rashford amefunga mabao 14 kwa United kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu na Solskjaer amesema klabu itafanya kila liwezekanalo kumsaidia nyota huyo mwenye umri wa miaka 22.

"Anapona haraka na anacheza akiwa na maumivu, kama anaweza naamini atakuwa kwenye kikosi chetu," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini tumeona kwamba, alikuwa na wakati mgumu, ila naamini atakuwa fiti tu kwa ajili yetu.

"Amekuwa na msimu bora zaidi, hivyo



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL YAKIRI KUKWAMA KUMNASUA AUBAMEYANG

### Arteta asema hakuna namna, sasa wajipanga kushuka dimbani bila uwapo wake huku...

**LONDON,** England

ARSENAL itamkosa Pierre-Emerick Aubameyang katika mechi tatu za baada ya kocha Mikel Arteta kuthibitisha kukwama rufani yao ya kuomba kuondolewa adhabu ya kadi nyekundu.

**Aubameyang alitolewa nje katika kipindi cha pili wakati Arsenal ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Crystal Palace Jumamosi baada ya kumchezea rafu mbaya Max Meyer.**

Nahodha huyo wa Arsenal, mwanzoni alionyeshwa kadi ya njano kwa kucheza rafu hiyo iliyoonekana ya kutodhamiria, lakini Teknolojia ya Kumsaidia Refa kwa njia ya Video (VAR), ilimwongoza mwamuzi Paul Tierney kubadili maamuzi na kuwa kadi nyekundu ya moja kwa moja.

Arsenal ilikatia rufani kadi hiyo nyekundu, lakini katika mkutano wake na waandishi wa habari kuelekea mechi ya Jumamosi dhidi ya Sheffield United 'Blades'- Arteta alifunguka kuwa Aubameyang atapaswa kutumikia adhabu yake.

"Kwamba imethibitishwa kuwa atatumikia adhabu ya kukosa mechi tatu, hivyo hatutakuwa naye katika michezo mitatu," Arteta aliwaambia wanahabari.

"Ni aibu kubwa, ni pigo kubwa kwetu kwa sababu tunafahamu halikuwa lengo lake. Lakini ilitokea kuwa rafu, maamuzi yakafanyika na tunapaswa kukubali hilo.

"Alihuzunika sana baada ya mchezo, kukatishwa tamaa kwa kuiacha timu na wachezaji 10. Lilikuwa tukio ambalo kwangu mimi ni wazi kabisa ni la bahati mbaya kwa maoni yangu.

"Kwangu mimi amekuwa bora, akijituma sana, akifunga mabao na pengine amekuwa mchezaji muhimu zaidi kwa timu, hivyo kumpoteza ni kweli ni habari mbaya kwetu."

Aubameyang, ambaye ataikosa mechi ya Jumamosi dhidi ya Blades, 'dabi' dhidi ya Chelsea na mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Bournemouth, aliifungia Arsenal bao la kwanza katika Uwanja wa Selhurst Park kabla ya Jordan Ayew kuisawazishia Palace.

## ZISIKUPITE

### BARKLEY AWINDWA WEST HAM

WEST Ham inapanga kutoa ofa ya kumnasa kwa mkopo kiungo wa Chelsea, Muingereza Ross Barkley, 26, ambaye alicheza chini ya Kocha wa Hammers, David Moyes pale Everton. ***(Mirror)***

### ERIKSEN, INTER WAKUBALIANA

INTER Milan imekubaliano malipo binafsi na kiungo Mdenrmark Christian Eriksen, 27, kuhusu kujiunga nayo jumla mwezi huu, lakini Tottenham inaitaka miamba hiyo ya Italia kutoa mara mbili ya ofa yao ya pauni milioni 8.5. ***(Calciomercato - in Italian)***

### SPURS KUMFUATA ZE LUIS

TOTTENHAM ipo katika mazungumzo ya kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa kimataifa wa Cape Verde, Ze Luis, 28, anayeichezea Porto. ***(Record - in Portuguese)***

### ARSENAL KUMUWAHI KURZAWA

ARSENAL inatazama uwezekano wa kutoa ofa ya pauni milioni sita kwa beki wa kushoto wa PSG, Layvin Kurzawa, 27, kabla ya kuwa mchezaji huru majira ya joto. ***(Sun)***

### CAVANI SOKONI ATLETICO

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Edinson Cavani, 32, atamaliza mkataba wake majira ya joto, lakini Paris St-Germain imeitaka Atletico Madrid kuongeza ofa yao ya euro milioni 10 hadi euro milioni 30. ***(Marca - in Spanish)***

### LIVER YAONGOZA KWA KAI

LIVERPOOL inajipanga kutoa pauni milioni 107 katika majira ya joto ili kuinasa saini ya kungo wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz, na inaongoza mbio hizo dhidi ya Manchester United, Barcelona na Bayern Munich zinazomwania pia nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 20. ***(Mundo Deportivo, via Mirror)***

### YOUNG AJIMWAMBAFAI INTER

BEKI wa kushoto wa Manchester United, Ashley Young, 34, anaamini Inter Milan bado itahitaji kumsajili hata kama wamemsajili Leonardo Spinazzola. ***(Sun)***

### OZIL AMFUNGUKIA EMERY

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil, 31, amesema alikuwa na "wakati mgumu" chini ya kocha wa hivi karibuni, Unai Emery lakini nyota huyo wa zamani wa kimataifa wa Ujerumani ni "mwenye furaha kwa kila kitu" chini ya Mikel Arteta. ***(Mirror)***

### DAKONAM ATESA VIGOGO EPL

ARSENAL na wapinzani wao, Tottenham ni miongoni mwa klabu tano za Ligi Kuu England zinazoiwania saini ya beki wa kati wa Getafe, Djene Dakonam. Monaco tayari ilishatoa ofa kwa beki huyo wa kimataifa wa Togo mwenye umri wa miaka 28, na kukataliwa. ***(Sun)***

### UNITED KUMFUATA LLORENTE

MANCHESTER United inataka kusajili kiungo wa kati kwa mkopo katika kipindi hiki cha msimu kilichobaki na Mhispania Marcos Llorente, 24, ambaye anaichezea Atletico Madrid, ameibuka kuwa mbadala. ***(Manchester Evening News)***

HABARI MICHEZO

# MAXIME ASHUKURU KUFUTA LAWAMA ZA KUIBEBA YANGA

**Na Mwandishi Wetu**

KIPIGO cha mabao 3-0 dhidi ya Yanga, kimeelezewa na Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, kuwa ni Mungu amejibu maombi yake baada ya shutuma za muda mrefu kuwa yeye ni shabiki wa timu hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam kutokana na mara nyingi kupoteza dhidi yao.

**Yanga ikiongozwa kwa mara ya kwanza na kocha wao mkuu, Mbelgiji Luc Eymael alierithi mikoba ya Mkongomani Mwinyi Zahera, ilikubali kipigo hicho katika Uwanja wa Uhuru juzi.**

Akizungumza na Nipashe juzi, Maxime alisema ameshatukanwa sana kuwa yeye anaifunga tu Simba, lakini akicheza na Yanga anafungwa, hivyo ushindi huo umejibu kilio chake cha muda mrefu.

"Kuna baadhi ya Watanzania sijui wana akili nusu, ukiifunga timu hii unaambiwa na nyingine wewe ni timu hii, kuifunga Yanga kwangu si rekodi bali Mungu mara nyingine huwa anageuza, nikikaa peke yangu huwa namlilia.

"Unajua mpira siku hizi huwa unaingiliwa, kuna siku utasikia hata Mmasai naye ni kocha, nishatukanwa sana naifunga Simba, Yanga inanifunga ukifunga timu hii unaambiwa wewe timu hii," alisema kocha huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar.

Alisema kwake yeye mpira huwa si kupaki basi bali huwaambia wachezaji wake "twendeni tukatumie mbinu hizi kama zikifanya kazi tutapata mabao kwa kuwa mpira kwao ni burudani.

Mchezaji huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar na Taifa Stars, alisema kilichompa ushindi mbele ya Yanga ni kujiamini na kuiruhusu timu yake kucheze bila hofu.

Alisema kawaida yake huwa hana hofu anapocheza na timu yoyote wakati wowote, jambo linalomfanya kupata matokeo na mbinu zao zikigundulika hufungwa.

"Ninapocheza na timu yoyote ninawaruhusu wachezaji kucheza na si kupaki basi ndio maana ikitokea ninashinda ninafunga kweli na nikibanwa ninafungwa kwa kuwa siruhusu kupaki basi," alisema.

Ushindi huo umeifanya Kagera Sugar kuvuna pointi zote tatu kwa mara ya kwanza kwenye mechi sita za Ligi Kuu zilizopita baada ya kushuka dimbani mara tano mfululizo na kuambulia alama moja tu.




Mwenyekiti wa Bodi ya Klabu ya Simba, Mohamed "Mo" Dewji (kulia) akiwa na Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Andres Sjoberg juzi, jijini Dar es Salaa katika mazungumzo yaliyohusu ushirikiano wa maendeleo ya soka la vijana. Mo Dewji amesema Balozi Sjoberg amejitolea kuleta makocha mashuhuri kuisaidia Simba kuanza mpango huo na kuzindua kituo cha kukuza soka la vijana cha klabu hiyo ndani ya mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

# Azam FC waanza tambo kwa Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Azam FC imeitumia salamu Yanga kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu watakaoucheza Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kesho.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha msaidizi wa Azam FC, Idd Cheche, alisema wana matumaini makubwa ya kuendeleza ushindani katika mchezo huo, na kwamba wataingia kwa tahadhari kubwa.

"Tumejipanga vizuri kuelekea katika mchezo wetu wa Jumamosi (kesho), lengo ni kupata pointi tatu na kuiweka timu yetu mahali pazuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu," Cheche alisema.

Hata hivyo, alisema mchezo huo utakuwa wa vuta nikuvute kutokana na ukweli kwamba timu hizo zinapokutana hutoa ushindani mkubwa kwa kuwa zote huundwa na wachezaji wazuri.

Kuhusu mechi yao ya juzi usiku dhidi ya Lipuli FC ambayo waliichapa mabao 2-0, Cheche alisema vijana wao walicheza kwa umakini mkubwa pamoja na kufuata maelekezo waliyowapa.

"Mchezo uliopita vijana waliweza kutumia vizuri maelekezo tuliyowapa, hali iliyotusaidia kutoka na pointi zote tatu," alisema.

Aliongeza kuwa hiki ni kipindi cha kuelekea kupata ubingwa, na kudai walitumia udhaifu wa wapinzani wao kupata ushindi huo.

Kwa matokeo hayo, Azam ambayo imeshuka dimbani mara 14 msimu huu, sasa imepanda hadi nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu ikiwa nyuma kwa alama moja dhidi ya washika nafasi ya pili, Coastal Union yeye pointi 30 baada ya kucheza mechi 17.

## Karia aula Caf

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Wallace Karia (pichani chini), amezidi kuula katika medali ya soka baada ya kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Maandalizi ya Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) ya Caf.

Desemba 18, mwaka jana, Karia alichaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Vyama vya Michezo vya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) katika uchaguzi mkuu uliofanyika nchini Uganda.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Cliford Ndimbo, kamati hiyo ambayo Mwenyekiti wake ni Rais wa Caf, Ahmad Ahmad, kazi yake itakuwa ni kuratibu fainali hizo.

Kadhalika, ilieleza kuwa Watanzania wengine wawili pia wamefanikiwa kuingia katika kamati hiyo ya Shirikisho la Soka barani Afrika.

Watanzania hao ni Dk. Paul Marialle, ambaye ameteuliwa kuwa mjumbe wa kamati ya tiba huku Lina Kessy yeye akiingia kamati ya mpira wa miguu wa wanawake.



## JKU yapania ubingwa Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU inayoshiriki Ligi Kuu ya Zanzibar, imesema imejipanga kufanya maajabu katika mzunguko huu wa pili, ili timu hiyo iweze kunyakuwa ubingwa msimu huu.

JKU ambayo ipo nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo baada ya kujikusanyia pointi 22, haikufanya usajili wa dirisha dogo ambao umefungwa hapo jana, Januari 15.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa timu hiyo, Sadu Ujudi, alisema malengo yao makubwa ni kuhakikisha wananyakuwa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu wa 2019-2020.

Alisema kikosi chake kipo vizuri na kina wachezaji wenye uwezo wa kujituma na kupambana uwanjani hivyo ana matumaini makubwa ya kuwa bingwa wa ligi hiyo.

Aidha, akizungumzia juu ya kikosi hicho kutofanya usajili wa dirisha dogo alisema hakuwa na haja ya kufanya usajili kwa kuwa tayari alishajaza idadi kamili ya wachezaji na wachezaji wote wanaviwango vinavyolingana.

# Michezo

Ijumaa Januari 17, 2020

Nipashe




Sarri aumia Messi kumzidi Ronaldo HABARI UK.28

HAMISHA...



Kiungo wa Manchester United, Fred (kushoto), akiokoa hatari wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Wolverhampton Wanderers kwenye mechi ya Raundi ya Tatu ya marudiano ya Kombe la FA iliyopigwa juzi usiku katika Uwanja wa Old Trafford baada ya ile ya awali, Januari 4 katika Dimba la Molineux kumalizika kwa sare tasa. Bao hilo pekee la United lilifungwa na Juan Mata katika dakika ya 67. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YACHANA MBAO KIRUMBA

## ●●● Mkude afungua msimu, Dilunga akiendelea kung'ara, sasa yaisubiri Alliance Jumapili huku...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO ya wachezaji wanaocheza nafasi za kiungo katika kikosi cha Simba, Hassan Dilunga na Jonas Mkude, yaliiwezesha timu hiyo kutwaa pointi zote tatu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza dhidi ya Mbao FC.

**Simba jana ilifanikiwa kuichapa Mbao mabao 2-1 kwenye mechi kali ya Ligi Kuu Tanzania Bara, ingawa iliharibiwa kidogo na uwanja ambao sehemu kubwa zilikuwa na madimbwi ya maji kutokana na mvua kubwa kunyesha jijini Mwanza tangu asubuhi.**

Mechi ilianza kwa kasi na dakika za mwanzoni tu, nusura Simba ipate bao, baada ya Shomari Kapombe kupiga krosi iliyokuwa ikiingia yenyewe, lakini kipa wa Mbao Abdallah Makanganya, aliipangua na kuwa kona.

Dakika ya 24, Mohamed Hussein 'Tshabalala,' aliikosesha timu yake bao la wazi alipopiga nje akiwa peke yake mpira uliotokana na krosi ya Dilunga.

Baada ya kuona hivyo, Dilunga aliamua mwenyewe kuambaa na mpira kutoka kwenye winga ya kulia na kuwapiga chenga mabeki wa Mbao, huku akitoka pembeni mwa uwanja na kuingia ndani kidogo, umbali wa mita kama 30 hivi kabla ya kuachia kombora kali la mguu wa kushoto na mpira ukajaa wavuni, ikiwa ni dakika ya 41.

Kuingia kwa bao hilo kulionekana kuwachanganya kidogo Mbao FC na kuwafanya Simba kutawala mechi hiyo kuanzia hapo. Dakika moja tu ya kipindi cha pili, Mkude aliandika bao la pili kwa Simba na la kwanza kwake kwa msimu huu, alipounganisha kwa mguu wa kulia mpira wa kona uliopigwa na Ibrahim Ajibu.

Straika wa Mbao, Waziri Junior ambaye alionekana kuwasumbua mno mabeki wa Simba, aliipatia timu yake bao dakika ya 53 baada ya kuunganisha kwa kichwa mpira wa faulo uliopigwa na Charles Emmanuel.

Nusura Mbao isawazishe bao la pili dakika ya 65 kama mpira wa krosi uliounganishwa kwa umaridadi mkubwa na Waziri usingetoka juu kidogo ya lango la Simba.

Ni kipindi ambacho Mbao ilicharuka na kufanya mashambulizi kadhaa makali langoni mwa Simba, lakini mabeki wa viungo wa timu hiyo walionekana kuwa makini na kujituma zaidi kwenye mechi hiyo kuliko kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Mtibwa Sugar, hivyo kuzima hatari hizo.

Dakika ya 85, Ajibu alimpisha Rashi Juma huku dakika chache kabla ya mechi hiyo kumalizika, mfungaji wa bao la kwanza, Dilunga aliumia na nafasi yake kuchukuliwa na Tairone Santos.

Kwa matokeo hayo Simba inazidi kujichimbia kileleni kwa kufikisha pointi 38, ikiwa imecheza mechi 15, ikishinda mechi 12, sare mbili na imepoteza mechi moja, huku Mbao ikisalia kwenye nafasi ya 14 na alama zake 18 baada ya kushuka dimbani mara 17, ikishinda nne, sare sita na kupoteza mechi saba.

Simba itashuka tena katika uwanja huo Jumapili kuivaa Alliance FC katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Bara.

# Mbelgiji Yanga achambua kipigo

**Na Mwandishi Wetu**

KUSHINDWA kutumia nafasi nne hadi tano walizozipata dhidi ya Kagera Sugar huku wakiruhusu mabao ya kizembe ndicho kilichochangia kipigo cha mabao 3-0 juzi katika Uwanja wa Uhuru, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael.

Mbelgiji huyo, aliyerithi mikoba ya Mkongomani Mwinyi Zahera, alisema wachezaji wake walipoteza nafasi nyingi za wazi jambo lililowasababishia kipigo hicho, katika mechi yake ya kwanza kuiongoza timu hiyo.

"Kipindi cha kwanza tulicheza soka nzuri na hutukuweza kufunga kwa kutumia nafasi nne hadi tano tulizozipata na tulicheza pungufu kutokana na mchezaji wetu [Mohamed Banka] kuonyeshwa kadi nyekundu.

"Kipindi cha pili walinzi wetu walifanya makosa [Kelvin Yondani na Lamine Moro] tukaruhusu bao la kijinga la kubabatiza, lakini pia hatukuwa wazuri ndani ya boksi," Eymael alisema.

Kocha huyo alisema hawakuwa na nafasi ya kupoteza bali kushinda kutokana na nafasi ambazo walizitengeneza kwenye mchezo.

Matokeo hayo yaliifanya Yanga kushuka nafasi moja hadi ya nane baada ya mechi 13 ikiwa na alama zake 25, wakati huu kesho ikijiandaa kuivaa Azam FC kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >